




**Auawa** kwa risasi akiokota kuni shambani

UKURASA 2




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Novemba 13, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581128

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




# Mkemia Mkuu atoa ripoti tope la mgodi lililovamia wananchi

• **Wananchi** kulipwa fidia... *Endelea ukurasa 2*



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Phillip Mpango, wakifurahia jambo wakati wa kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilichofanyika jana Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma. Kulia, ni Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza kikao hicho. **PICHA: IKULU NA CCM**

## TAKUKURU yabaini tatizo katika miradi ya mabilioni

UKURASA 5



## Itakachokivuna Tanzania ziara ya Rais Samia China, Misri

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA KAZI ILE ILE KWA KAGERA SUGAR UK.24 **KATUNI** UK.6

# Mkemia Mkuu atoa ripoti tope la mgodi lililovamia wananchi

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ( NEMC) limesema maji na tope yaliyotokana na kubomoka kwa kingo za bwawa la Mgodi wa Williamson Diamonds hayajaleta athari kwa mazingira na viumbe hai baada ya kupokea uchunguzi wa awali kutoka ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samwel Gwamaka alibainisha hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea baadhi ya maeneo ambayo yameathiriwa na maji na tope la bwawa hilo.

Alisema uchunguzi wa awali kutoka kwa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali haujaonyesha athari zozote kwa mazingira na viumbe hai na kuwataka wananchi waliokumbwa na tukio hilo kuwa watulivu wakati serikali ikiendelea na uchunguzi zaidi.

"Sampuli zilizopelekwa kwa Mkemia Mkuu zimeonyesha maji na tope hili halijaleta athari kwa mazingira na viumbe hai. Tunasubiria ripoti ya Tume ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga ili tuweze kuchukua hatua zingine za kisheria," alisema Dk. Gwamaka.

Mkurugenzi huyo alisema mgodi huo utawajibika kulipa fidia kwa wananchi waliopatwa na janga hilo pamoja na kurekebisha miundombinu iliyoharibiwa ikiwamo mashamba ya wananchi na nyumba ambazo zimepatwa na kadhia hiyo.

"Uharibifu wa mazingira uliosababishwa na tukio hili ni mkubwa, ni lazima wawajibike kuhakikisha mazingira yanatunzwa, hatua walizochokua za kusimamisha shughuli za uzalishaji na matumizi ya bwawa zinapaswa kuzingatiwa ili lisije kuleta madhara zaidi kwa wananchi," alisema.

Meneja Mkuu wa Mgodi wa Williamson Diamods, Ayoub Mwenda alisema kuwa kwa sasa wanaendelea kujenga uzio ili kuyadhibiti maji hayo yasisambae kwenye makazi ya watu hususani wakati huu ambao mvua imeanza kunyesha kwa wingi mkoani Shinyanga.

"Tunajenga matuta ili kuyadhibiti maji haya yasiendelee kusambaa, wataalamu wetu wanafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha maji hayo yanadhibitiwa," alisema Mwenda.

Aliongeza: "Mpaka sasa mgodi unaendelea kuwahudumia waathirika wa tukio hili wapatao 115 wakati tunasubiria majibu ya tume na tutahakikisha wanapata stahiki zao zote ikiwamo chakula na malazi huku watoto wao nao wakipelekwa shuleni kama kawaida."

Baadhi ya wakazi ambao wameathirika na tukio hilo, akiwamo Juma Masele, waliishukuru serikali kwa kuchukua hatua dhidi ya tatizo hilo na kuiomba kuwasaidia eneo lingine ili waendelee na kilimo wakati huu ambao mvua imeanza kunyesha.

"Baadhi yetu ni wakulima, wafugaji na wachimbaji wa madini, tunaomba tupatiwe eneo lingine ili tuweze kuendelea na kilimo kwani kuendelea kukaa kwenye kambi hii wakati mvua inanyesha itakuwa tunapoteza muda," alisema Masele.

**USULI NA HISTORIA**

Inaporejewa historia ya uchimbaji madini Tanzania, kuwapo almasi kwenye eneo la Mwadui kuligunduliwa mwaka 1940 na raia wa Canada, Dk. John Williamson, mtaalamu wa jiolojia aliyekuwa amebobea katika masuala ya madini.



Kaimu Mkuu wa Idara ya Sheria Ofisi ya Haki Miliki Tanzania, Zephania Lyamuya (wapili kushoto) akitoa elimu kwa waandishi wa habari wa IPP MEDIA katika Ofisi ya The Guardian Ltd, Mikocheni Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja Rasilimali Watu wa Kampuni ya The Guardian Ltd. Emmanuel Matondo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mkufunzi atoa hadhari kwa wanaonyonyesha

**Na Romana Mallya**

MKUFUNZI wa Mazoezi kutoka Shirika la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (NCD), Dk. Waziri Ndonde amesema katika kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza kwa mwanamke anayenyonyesha mwenye uzito kupita kiasi, anatakiwa kutumia dakika 150 kwa wiki kufanya mazoezi.

Dk. Ndonde alitoa angalizo hilo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza kilichofanyika mkoani Mwanza na kudhuriwa na watu mbalimbali.

Alisema dhana kubwa ya kujikinga na kuzuia magonjwa hayo ni pamoja na kuzingatia masuala ya lishe, kutokutumia tumbaku na kuushughulisha mwili kwa kufanya mazoezi.

"Kuushughulisha mwili na kufanya mazoezi ni kitu cha msingi cha kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza, pamoja na lishe, ukiwa na tabia bwete, kuishi bila kuushughulisha mwili ni moja ya sababu ya kupata magonjwa haya," alisema.

Mtaalamu huyo alisema serikali katika kutambua hilo, mwaka jana kwenye wiki kama hiyo, Wizara ya Afya ilizindua mwongozo wa kushughulisha mwili na kufanya mazoezi katika kuepuka tabia bwete.

"Mwongozo huu tayari umeshachapishwa na wadau mbalimbali wamepewa wanaendelea kupata elimu, moja ya lengo kubwa la wiki hii kwa mwaka huu ambapo tunaadhimisha hapa Mwanza, ni kuelimisha watu zaidi mapendekezo ambayo yapo ndani ya mwongozo huo," alisema.

Aliongeza kuwa mwongozo upo wazi kwa watu wa rika zote, mfano wenye magonjwa sugu na wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU), umeelekeza namna gani ya kuushughulisha mwili kwa kufanya mazoezi.

Pia alisema kulikuwa na shida nyingi kwa wajawazito na waliojifungua, zinazotokana na mila na desturi wanakuwa na uzito uliokithiri baada ya kujifungua kutokana na lishe wanayopewa.

"Mwongozo unamtaka huyu mama atumie angalau dakika 150 kwa wiki wakati anatunzwa kupewa chakula bora ili apate maziwa ya kumnyonyesha mtoto, dakika hizo azitumie kwa wiki kuhakikisha hatapata unene uliokithiri, dakika hizo atatakiwa kufanya mazoezi yote muhimu," alisema.

Pia alisema mwongozo huo umetoa maelekezo kwa wazee, yaani watu wenye umri wa zaidi ya miaka 65, kuhusu nini wanapaswa kufanya ili kuepuka magonjwa hayo.

# Auawa kwa kupigwa risasi akiokota kuni katika shamba

**Na Oscar Assenga,** MUHEZA

MTU mmoja wilayani Muheza mkoani Tanga amefariki dunia baada ya kudaiwa kupigwa risasi kifuani na mlinzi wa shamba la Magoroto Estate wilayani Muheza, Samson Steven wakati akiokota kuni kwenye shamba hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Henry Mwaibambe alithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema kuwa kufuatia tukio hilo, wanamshikilia Samson Steven ambaye ni mlinzi wa shamba hilo kwa tuhuma za kuhusika na mauaji hayo.

Kamanda Mwaibambe alimtaja marehemu aliyepigwa risasi wakati akiokota kuni ni Athumani Ramadhani ambaye baada ya kupigwa risasi ya kifuani alifariki dunia papo hapo.

"Kwa kweli hili ni tukio la kusikitisha na hivi sasa Jeshi la Polisi tunamshikilia mtuhumiwa ili kujibu tuhuma zinazomkabili za kufanya mauaji kwa raia," alisema Kamanda Mwaibambe.

Kiongozi huyo alisema kuwa maelezo ya mtuhumiwa ni kwamba alimpiga risasi ikiwa ni sehemu ya kujihami baada ya kumkamata kwa kuingia kwenye shamba hilo kinyume cha taratibu.

Alisema mtuhumiwa huyo katika maelezo yake kwa polisi, alidai wakati akijaribu kumtia nguvuni, alitaka kumvamia na ndiye alifyetua risasi.

Kamanda huyo alitoa wito kwa wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi kwa kuwa iwapo kunatokea vitendo vya uhalifu, wanapaswa waripoti kwenye mamlaka husika ili zichukue hatua.

Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania toleo la mwaka 1977, inaeleza: "Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria".

## HABARI KITAIFA

# Itakachovuna Tanzania ziara ya Rais Samia China na Misri




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akizungumza na wataalam pamoja na wadau wa afya jijini Dar es Salaam hivi karibuni wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya utayari kupambana dhidi ya ugonjwa wa Ebola yatakayofanyika kwa siku 4 katika Wilaya 5 za Mkoa wa Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Na Romana Mallya**

MAWAZIRI na maofisa wa serikali wamebainisha fursa za kiuchumi itakazonufaika nazo Tanzania kutokana na ziara ya hivi karibuni ya Rais Samia Suluhu Hassan katika nchi za China na Misri.

Watendaji hao wa serikali walibainisha manufaa hayo katika mkutano maalum wa mahojiano na waandishi wa habari uliofanyika jana Ikulu jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Suleiman Jafo.

Viongozi wengine walioshiriki ni Balozi wa Tanzania China, Mbelwa Kairuki, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka huku mkutano huo ukiongozwa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus.

Katika mkutano huo, watendaji hao walitaja mafanikio kadhaa yatokanayo na ziara hiyo iliyofanyika kwa siku tatu kuanzia Novemba 2 mwaka huu huku wakiwataka Watanzania kumuunga mkono Rais Samia kwa kutunza mazingira ili fursa zinazojitokeza utekelezaji wake ulete tija kwa taifa.

Akitaja mafanikio ya ziara hizo kwa kuanzia na ile ya China, Zuhura alisema wamekubaliana kuendeleza kushirikiana katika masuala ya kimataifa na kikanda na kukubaliana kupandisha hati ya uhusiano ili kuwa na ushirikiano wa kina na kimkakati.

Kiuchumi, Zuhura alisema wamekubaliana kushirikiana katika kuongeza zaidi bidhaa kutoka Tanzania kwenda China hasa za kilimo, mifugo na uvuvi na nchi hiyo imeahidi kutozitoza ushuru kwa asilimia 98.

"China imeahidi kuongeza uwekezaji Tanzania kupitia kampuni zake katika mnyororo wa kiuchumi na kijamii, zimekubalina ushirikiano katika ujenzi wa viwanda ili kuiongezea Tanzania uwezo wa uzalishaji, usindikaji na utengenezaji wa bidhaa," Zuhura alisema.

Pia alisema wamekubaliana kushirikiana katika uchumi wa kidigitali, uchumi wa bluu na maendeleo ya kijani na China imekubali kuiunga mkono Tanzania kutekeleza mradi wa kufufua reli ya TAZARA.

Katika ulinzi na usalama, Zuhura alisema nchi hizo zimekubaliana kuimarisha ushirikiano na kudumisha amani na masuala ya kijamii na kwamba mwaka 2024 nchi hizo zitaadhimisha miaka 60 ya uhusianao wa kidiplomasia, hivyo wamekubaliana uwe mwaka wa utalii na utamaduni.

Zuhura pia alisema China imeahidi kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Tanzania na kupeleka timu za matibabu Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Pia alisema wamekubaliana kuongeza ushirikiano wa kimataifa na kulifanyika utiaji saini hati za makubaliano 15 ya mikataba na itifaki, ikiwamo fursa kwa wakulima hasa wa parachichi.

"Pili, wavuvi wa Tanzania hasa wanaouza mabondo ya samaki, sekta ya utalii wametia saini mkataba wa kupata manufaa ya kujenga makumbusho ya kisasa ya kutunza nyayo ya binadamu wa kwanza mwenye umri wa miaka milioni tatu, zilizopo Hifadhi ya Ngorongoro.

"Sekta ya mawasiliano wamekubaliana kujenga uchumi wa kidigitali, Tanzania itapata teknolojia mpya ya mawasiliano ya 5G, hati nyingine ni ya uchumi wa bluu ambayo wamekubaliana kukuza uchumi na utaalamu na Tanzania imepatiwa fedha za China (Yuan) milioni 100.

"Walitia saini mkataba wa Uwanja wa Ndege Zanzibar na hati ya makabidhiano vya upekuzi kwa viwanja vya ndege Tanzania Bara," alisema.

Pia alisema vipo vikosi kazi vimeundwa mahususi kushughulikia masuala ya biashara na uwekezaji baina ya nchi hizo.

Kupitia mkutano wa COP27 unaofanyika nchini Misri, alisema mbali ya makubaliano ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi, kulikuwa na suala la kuchapusha miradi ya kupunguza hewa ukaa.

Alisema kulikuwa na uzinduzi wa kujenga uwezo wa mtandao wa kuunganisha gridi za umeme Nchi za Kusini mwa Afrika pamoja na nishati jadidifu, mahususi kwa ajili ya kuvutia wawekezaji kuzalisha nishati hiyo kwa wingi na kwa bei nafuu kwa kuzingatia utunzaji mazingira.

Mkutano huo ambao Rais Samia alikuwa mwenyeji, alipata ushirikiano kutoka kwa marais wengine wa Zimbabwe, Zambia, Botswana, Malawi, Makamu wa Rais wa Angola na taasisi mbalimbali za dunia.

Alisema kupitia mkutano huo, Tanzania imeahidiwa dola za Marekani bilioni 18 kutoka Benki ya Dunia (WB) kwa ajili ya miradi ya nishati jadidifu ikiwamo miundombinu na usafirishaji umeme.

"Marais nao wamekubaliana kuongeza kasi kwenye miradi ambayo itaunganisha nishati kutoka nchi moja kwenda nyingine na kutoa ushirikiano unaohitajika ngazi ya kitaifa, Tanzania ina banda maalum katika mkutano huo," alisema.

Kuhusu ujenzi wa kufua umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, Zuhura alisema viongozi wa pande zote wameridhishwa na wametaka utekelezwe kwa ubora stahiki.

Kuhusu fursa ya soko la parachichi, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Nchemba, alisema ziko hatua kubwa zinazochukuliwa ikiwamo kuwa na mbegu bora na za kisasa ili zao hilo liwe kwa viwango vya mahitaji ya masoko. Alisema wanaimarisha masuala ya kimfumo kwenye uingizaji wa bidhaa ili kupunguza usumbufu katika masuala ya kukadiria kwa macho.

Akizungumzia mazingira, Waziri Jafo alisema watanzania wanatakiwa kufahamu kuwa suala hilo si la viongozi bali la kila mtu.

Waziri Jafo alisema nchi zilizoendelea zinaongoza kwa uchafuzi wa mazingira na kilio cha nchi zinazoendelea ni zitimize wajibu wao wa kutoa fedha dola bilioni 100 kutekeleza miradi ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi ingawa utekelezaji wa hilo hauridhishi.

"Katika kipindi kilichopita Tanzania ilipokea dola milioni 23.6. Kwa mwaka huu mgawo unaokuja utakuwa ni dola milioni 52.8, hivyo itakuwa imeongezeka kidogo baada mkutano ule wa COP26 mwaka jana, ili tupambane na mabadiliko ya tabianchi. "Uchomaji wa moto tumeshuhudia misitu Amazon ikiwaka, ukiona inawaka ujue dunia nzima inaathirika, ukiona Mlima Uluguru unawaka moto, dunia nzima inaathirika, vivyo hivyo Mlima Kilimanjaro ukiungua.

"Niwaombe watanzania ajenda ya kupambana na moto, sote tuepuke kuchoma, si Mlima Kilimanjaro tu, bali mahala popote.

"Wengine wanalifanya ni suala la utamaduni eti akichoma moto ukienda mbali inaashiria ataishi muda mrefu kumbe si kweli," alisema.

Dk. Jafo alisema hali kwa sasa katika wilaya za Longido, Kiteto na Simanjiro ni mbaya, akibainisha wanyama wanaofugwa na wanyamapori wameathirika.

Alisema hali hiyo pia inashuhudiwa hadi Kenya, mifugo na wanyamapori wanakufa kutokana na kukosa malisho na maji, hivyo akawataka watanzania walinde vyanzo vya maji na kutunza mazingira na wasichome moto, bali wapande miti.

Waziri Tax aliwakumbusha wafanyabiashara kuwa biashara yoyote ina mambo matatu -- ubora, wingi na upelekaji kwa wakati eneo husika.

Balozi Kairuki alisema: "Mwaka juzi Tanzania na China zilitia saini mkataba wa kuruhusu soya ya Tanzania kuuzwa China. Tangu kutiwa saini (mkataba huo), tayari kuna kampuni za Tanzania 103 zimesajiliwa na zinauza soya China, tumeuza tani 1,161 na mahitaji ni tani milioni moja, China imekubali kuwajengea uwezo wakulima wa Tanzania."

Alisema hivi karibuni Wizara ya Kilimo itatia saini makubaliano na taasisi ya China ambayo hakuitaja kwa jina, akiwa na ufafanuzi kwamba wakulima watapata pembejeo na soko la uhakika na awamu ya kwanza itahusisha mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Njombe na Iringa.

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**ILIYOPO SHINYANGA**

**MAOMBI MADOGO YA MADAI NA. 37 YA 2022**

**KISHEGENA TRANSPORT LIMITED**

**DHIDI YA**

1. **AZANIA BANK LIMITED**
2. **MABUNDA AUCTIONEER MART CO. LTD**
3. **MEK ONE INDUSTRIES LTD**
4. **ATTORNEY GENERAL**

**KWA: MABUNDA AUCTIONEER MART CO. LTD**

**POPOTE ULIPO**

Unajulishwa kwamba mnamo tarehe 15/11/2022 saa 3:00 asubuhi imepangwa kusikilizwa kwa rufaa dhidi yenu.
Hivyo unaamriwa kuhudhuria siku hiyo bila kukosa na kama hutahudhuria rufaa hiyo istasikilizwa na kutolewa uamuzi bila nyinyi kuwepo.
Imetolewa kwa amri yangu na kupigwa chapa ya Mahakama leo tarehe 7/11/2022.

THE HIGH COURT OF TANZANIA

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA SHINYANGA

**RIPOTI MAALUM-2**

# Wavuvi wanavyouhusisha uhaba wa samaki na dhambi

**Na Mary Geofrey aliyekuwa**
MTWARA

**JANA katika sehemu ya kwanza ya ripoti hii, kulikuwa na ushuhuda wa shida zinazowakabili wavuvi na wachuuzi wa samaki katika Soko la Feri mkoani Mtwara kutokana na uhaba wa samaki uliolikumba eneo lao. Endelea na sehemu ya mwisho kupata undani wa kinachowasibu.**


Wavuvi katika Soko la Feri mkoani Mtwara wakiwa wameegesha vyombo vyao kusubiri muda wa kazi wiki iliyopita. **PICHA ZOTE: MARY GEOFREY**

KILIO cha uhaba wa samaki katika Soko la Feri pia kinasikika kutoka kwa Dalali wa Samaki, Said Omary anayebainisha kuwa tangu kuadimika kwa bidhaa hiyo, kipato chake kimeshuka kutoka wastani wa Sh. 100,000 hadi Sh. 40,000 kwa siku.

"Na hii inategemea boti imeenda na kurudi mara ngapi lakini siwezi kulinganisha nilichokuwa ninapata awali na sasa. Miaka ya nyuma nilijenga na nilimudu vizuri kuhudumia familia ila sasa tunapata riziki kidogo," anasema.

Dalali huyo anasema sababu ya kuadimika samaki ni kuwapo anachokitaja mabadiliko ya bahari ambayo chanzo chake ni watu kufanya uharibifu wa kukata miti na uvuvi haramu.

Mfaume Mangoda, mfanyabiashara wa samaki katika kizimba kwenye eneo la soko hilo, anasema samaki wa kilo 2.5 anawanunua kwa Sh. 20,000 na kuuza kwa Sh. 23,000 hadi Sh. 25,000.

"Samaki wameadimika, wavuvi hawana vifaa vya kisasa vya kuvua samaki, serikali ijitahidi kununua boti na meli zinazowezesha uvuvi wa kina kirefu," anashauri.

**WAVUVI NA DHAMBI**

Mvuvi Abdallah Hamadi (42) anaamini kuwapo dhambi na mambo ya yasiyompendeza Mungu yanayoendelea duniani, kumesababisha Mungu aamue kushusha adhabu ya kuadimika kwa samaki.

"Tuache dhambi, turejee kwa muumba wetu. Yeye ndiye kila kitu kwenye maisha yetu, tusipofanya hivyo, kila kitu kitabadilika maishani mwetu," anaonya Hamadi na kubainisha kuadimika huko kwa samaki kumebadili mfumo wa kipato, kazi yake na maisha kwa ujumla.

Anakumbusha alianza shughuli za uvuvi miaka 22 iliyopita wakati huo walitumia saa moja na nusu hadi saa mbili kwenda na kurudi kutoka baharini kuvua samaki na walikuwa na uhakika wa kupata samaki wa kujaa ndoo 70 zenye ujazo wa lita 10 na kuwauza mnadani, wakigawana Sh. 15,000 hadi 20,000 kila mmoja.

"Kwenye mtumbwi mmoja tunakuwa wavuvi 15 ambao tukishavua na kurudi nchi kavu samaki wanapigwa mnada na hapo unakuta tunagawana kila mmoja kiasi hicho cha fedha kwa safari moja. Kwa siku tulikuwa na uwezo wa kuondoka na Sh. 70,000 hadi 100,000 kila mmoja.

"Sasa hali ni tofauti kwa sababu tunatumia saa tatu kufika eneo lenye kina kirefu wanakopatikana samaki na kuvua. Kuna wakati hatupati samaki wa kutosha, tunaambulia ndoo tano hadi 10 na kupata Sh. 15,000 hadi 20,000 kila mmoja kulingana na wingi na ukubwa wa samaki tuliopata siku hiyo," anasema.

Mfanyabiashara wa Samaki, Aisha Mikidadi anazitaja imani potofu za kishirikina na matukio mabaya ya mauaji ya binadamu yanayofanyika baharini, yanasababisha kuadimika kwa viumbe hao.

Anasema kuwa ili kupata samaki kwa wingi kama ilivyokuwa awali, watu wanapaswa kuacha uovu ili Mungu aachilie baraka zake zilizokuwapo.

"Kila kukicha mauaji, balaa hazipungui, kafara, wanaume wanakuwa kama wanawake na wanawake kama wanaume na mambo mengine ambayo dunia inastaajabu. Kweli bado bahari nayo iwe sawa?" Aisha anahoji.

**UONGOZI SOKONI**

Mwenyekiti wa Wafanyabishara wa Soko la Samaki Feri, Mwinyi Mzaina anayataja mabadiliko ya tabianchi kuwa kiini cha kuadimika kwa samaki, akifafanua kuwa msimu wanaotarajia kupata samaki kwa wingi, hawawapati lakini wanawapata kipindi ambacho hawana matarajio hayo.

Kiongozi huyo pia anasema ongezeko la wavuvi nalo limechangia kuadimika kwa samaki, akiwasilisha takwimu kwamba sasa Manispaa ya Mtwara inao 1,025 na mkoa mzima wana wavuvi 6,400.

"Kuna ongezeko kubwa la vijana wasio na leseni wanaovua samaki kinyemela, ndiyo sababu samaki kuendelea kupungua kwenye maji ya kina kifupi na kukimbilia maji ya kina kirefu," anasema Mzaina na kutaja hatua wanazochukua zinajumuisha kutoa elimu kwa wavuvi na kuzuia shughuli za uvivu haramu ili kuepuka mabadiliko ya tabianchi yanayoleta athari kubwa.

Ofisa Mazingira Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, Tumaini Mosha, anasema samaki wameadimika kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

"Haya ni moja ya madhara yake, samaki wameadimika katika eneo la bahari, wanakimbilia maji ya kina kirefu na hivyo wavuvi kukosa mazao ya kutosha ya samaki," anasema na kukiri kuwapo tatizo la uvivu haramu ukiwamo wa kutumia mabomu na hivyo kuua mazalia ya samaki walio katika kina kifupi cha maji.

"Elimu inaendelea kutolewa kwa wananchi wanaofanya shughuli zao kando ya bahari kuendelea kuitunza na kuepuka shughuli zinazochangia kuwapo kwa tatizo hilo," anasema.

Nipashe pia inatua mezani kwa Ofisa Uvuvi Mkoa wa Mtwara, Emelitha Sauro, anayekiri kuadimika kwa samaki katika eneo hilo la bahari anakokutaja kunachangiwa na mabadiliko ya tabianchi kutokana na ukataji wa miti ya mikoko eneo la bahari na uvuvi haramu. Anasema miti hiyo ni chanjo cha chakula cha samaki.

Katika kukabiliana na uhaba wa samaki mkoani Mtwara, ofisa huyo anasema wamechukua hatua kuhakikisha wavuvi wanakuwa na vyombo vya kisasa vya uvuvi na kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wameweka mipango ya kupeleka boti za kisasa kwa ajili ya wavuvi.

Anasema wanashirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo ambayo imeingia mkataba na wizara kwa lengo la kuwakopesha wavuvi boti za kisasa na kuinua kipato chao huku wakiwataka wavuvi kuachana na mitumbwi ya mbao ambayo hutumia miti mingi kuitengeneza na hivyo, kuendelea kuharibu mazingira. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, kupitia hotuba yake ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka huu wa fedha ya Mei mwaka huu, alibainisha sekta ya uvuvi inanufaisha zaidi ya watu milioni 4.5 nchini, huku ikichangia asilimia 1.8 kwenye Pato la Taifa.

Alibainisha kuwa hadi Aprili 30 mwaka huu, tani 34,841.72 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo vipande 169, 089 viliuzwa nje ya nchi na kuliingizia taifa Sh. bilioni 475.01.

Waziri Ndaki pia alibainisha kuwa shughuli za uvuvi nchini zinafanywa zaidi na wavuvi wadogo kwenye maji ya asili, ambao huchangia takriban asilimia 95 ya samaki wote wanaovuliwa nchini kupitia vyombo vya uvuvi vipatavyo 57,991.


Wachuuzi wa samaki wakisubiri bidhaa kwenye soko hilo wiki iliyopita.

# Rais Samia awaita mabalozi wote nchini

Na Mwandishi Wetu

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaita mabalozi wote wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali kwenye mkutano maalum utakaofanyika visiwani Zanzibar kuanzia Jumatatu kwa kaulimbiu ya 'Mpya Katika Kuimarisha Diplomasia ya Uchumi.'

Akizungumza na Wahariri wa vyombo vya habari jana, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax alisema mkutano huo utaanza Novemba 14 hadi 21 mwaka huu.

Katika taarifa yake iliyosomwa kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mind Kasiga, alisema lengo la mkutano huo ni kutoa fursa kwa mabalozi na watendaji wa wizara wanaoshiriki katika uratibu wa utekelezaji wa sera ya mambo ya nje kupokea maelekezo ya Rais.

Maelekezo hayo ni kuhusu mwelekeo wa serikali katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi, kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi, kuainisha kero katika utekelezaji wa majukumu na kuja na mikakati madhubuti ya namna ya kuzitatua kero mbalimbali za kiutendaji, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

"Mkutano huu ni fursa kwa Tanzania kuandaa mikakati ya pamoja ya namna ya kujiweka sawa (repositioning) ili kuhakikisha taifa linanufaika ipasavyo kutokana na fursa mbalimbali zilizopo katika maeneo ya uwakilishi.

"Nitafungua kikao cha mabalozi, Konseli Wakuu na Menejimenti ya Wizara Novemba 14, kitaenda hadi Novemba 17 mwaka huu. Katika siku hizo tumealika wadau mbalimbali wa sekta ya umma na binafsi kuongea na waheshimiwa mabalozi masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa majukumu yao," alisema.

Aliongeza kuwa Novemba 17, mabalozi na menejimenti ya wizara watatembelea vivutio vya utalii na miradi ya maendeleo ya kimkakati Zanzibar ikiwa ni pamoja na bandari za Malindi na Manga Pwani.

Novemba 18 kutakuwa na mkutano kati ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mabalozi na Menejimenti ya Wizara.

Alisema Novemba 19 Rais atakutana na mabalozi na watendaji hao ili kuwa na majadala wa kina wa kuinufaisha nchi na wananchi wake.

Waziri Tax alisema: "Mabalozi wetu wote kutoka balozi zote 45 wanaoiwakilisha nchi yetu nje ya nchi watakuwapo nchini na moja ya majukumu waliyoelekezwa ya kufanya wakiwa nchini ni kujulisha umma kuhusu utekelezaji wa majukumu yao."

Huu ni mkutano wa kwanza kwa serikali hii kukutana na wanadiplomasia hao, viongozi waliopita walifanya hivyo kwa mwaka mara moja. Wakati wa uongozi wake, Dk. John Magufuli (hayati) alikutana nao mara mbili baada ya kuingia madarakani.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo akijibu maswali ya waandishi wa habari pamoja na kuelezea mafanikio yaliyopatikana kufuatia ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan China na Misri wakati wa mkutano uliofanyika jana Ikulu jijini Dar es Salaam. PICHA: OMR

# TAKUKURU yabaini tatizo miradi ya bil 4/-

Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Singida imechunguza miradi 11 yenye thamani ya Sh. bilioni 4.1 inayotekelezwa mkoani hapa na kubaini upungufu kadhaa ikiwamo baadhi ya malipo kufanyika kabla vifaa kupelekwa kwenye mradi husika.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Mzalendo Widege alibainisha hayo jana alipotoa taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu.

Alisema taasisi hiyo ilifanya uchunguzi katika miradi ya elimu, afya na maji ikiwamo ile ambayo inatekelezwa kwa fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Widege alisema katika uchunguzi wa miradi hiyo, wamebaini upungufu wa kuchelewa kukamilika kwa mujibu wa mkataba, baadhi ya taarifa kutojazwa kwa usahihi kwenye vitabu vya mapokezi na matumizi ya vifaa na malipo kufanyika kabla ya vifaa kupokewa kwenye mradi husika.

Kuhusu mfumo wa usimamizi wa mapato yanayokusanywa kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato (POS), alisema TAKUKURU imebaini baadhi ya stakabadhi zinazotolewa na wakusanyaji mapato hazitambuliwi kwenye mfumo wa kielektroniki wa Halmashauri ya Manispaa Singida na hivyo kusababisha mapato kupotea.

Upungufu mwingine uliobainika ni baadhi ya wakusanyaji wa mapato katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida kutowasilisha makusanyo benki kwa wakati na wengine kukusanya mapato kidogo katika eneo husika.

Widege alisema katika kipindi hicho, TAKUKURU ilipokea malalamiko 105 ambapo kati ya hayo, taarifa za rushwa zilikuwa 69 na zisizo za rushwa ni 36.

Aliongeza kuwa taarifa 69 zinazohusu rushwa zimeshughulikiwa kwa kuanzishiwa uchunguzi kwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

"Pia katika kipindi hiki, jumla ya mashauri sita mapya yamefunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya mashauri yanayoendelea mahakamani kufikia 27 ambapo shauri moja limeamuliwa," alisema.

# Wakusanyaji wa mapato wapewa onyo visingizio

Na Thobias Mwanakatwe, IKUNGI

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida limewataka watendaji kuacha kutoa visingizio visivyo na maana katika suala la ukusanyaji wa mapato badala yake washirikiane na madiwani ili kufikia malengo yaliyowekwa na halmashauri.

Madiwani wa halmashauri hiyo walitoa angalizo hilo jana wakati wa kikao cha baraza hilo, wakibainisha kuwa baadhi ya watendaji wamekuwa wakitoa visingizio vinavyosababisha kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato ambavyo vingi havina uhalisia.

Katika taarifa za ukusanyaji wa mapato kwa kila kata zilizosomwa na madiwani kwenye kikao hicho ambazo ziliandaliwa na watendaji wa kata, baadhi ya visingizio vilivyoelezwa ni pamoja na madai kwamba baadhi ya wafanyabiashara wanasafirisha mazao usiku, hivyo kukwepa kulipa ushuru.

"Tusiwe na visingizio katika ukusanyaji mapato, madiwani bila kusimama imara tutapata hasara, tuweke mikakati na sitegemei diwani aseme mapato fulani yasikusanywe," alisema Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Ally Mwanga.

Kiongozi huyo alisema suala la ukusanyaji mapato liwe la 'kufa na kupona' kwa kuhakikisha viongozi kuanzia ngazi za vijiji na kata wanasimamia na sio kuruhusu visingizio visivyokuwa na tija.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi alisema halmashauri inawategemea madiwani katika kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa kuwa wao wako kwenye vyanzo vya mapato.

"Mapato ya halmashauri ndiyo moyo wa halmashauri, kwa hiyo waheshimiwa madiwani kwenye vikao vya Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) mtusaidie kuweka msisitizo katika suala la ukusanyaji mapato," alisema.

Kijazi alisema Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi imepiga hatua kubwa katika suala la ukusanyaji mapato kwa kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, bajeti ya mapato ilikuwa Sh. milioni 900 tu lakini sasa bajeti imefikia zaidi ya Sh. bilioni mbili.

Diwani wa Ihanja, Mohamed Igae alisema ili kuongeza ukusanyaji mapato, halmashauri iwe na utaratibu wa kupeleka mashine za kukusanyia mapato (POS) katika kila kijiji badala ya hivi sasa ambapo zipo kwenye kata tu.

"Unakuta kijiji kipo mbali sana na makao makuu ya kata na mtendaji ndiye ana hiyo POS, sasa ni vigumu kwa mfano mfanyabiashara anataka kutoa ushuru wa mazao umwambie asubiri kwanza POS iletwe kutoka Km 50 au zaidi ili akatiwe stakabadhi," alisema.

Diwani wa Mwaru, Idd Makangale alisema katika kata hiyo kuna uchimbaji wa madini kwa muda mrefu lakini bahati mbaya halmashauri haikusanyi kodi kupitia uchimbaji huo na hivyo kutaka ukusanyaji uanze kufanyika.

Makangale pia alitaka ushuru wa Sh. 1,500 wa ukwaju uongezwe na kufikia Sh. 2,000 kwa kuwa zao hilo ni muhimu sana na linazalishwa kwa wingi katika kata hiyo.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu wa fedha, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi imefanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. milioni 707 sawa na asilimia 29 ya makusanyo.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Agizo la uondoshaji mifugo Mto Ruvu lifanyike haraka

**RAIS** Samia Suluhu Hassan juzi alizindua mradi wa maji, mitambo ya kuchimba visima na ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya kutatua tatizo la maji katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, huduma ambayo kwa sasa inatolewa kwa mgawo.

Pamoja na uzinduzi huo, Rais Samia alionyesha kushtushwa na ongezeko la mifugo katika Mto Ruvu ambalo linasababisha upungufu wa maji katika chanzo hicho ambacho ni tegemeo kwa wananchi wa mikoa hiyo.

Rais Samia alibainisha kuwa katika eneo hilo kuna zaidi ya ng'ombe 5,000 ambao licha ya kuharibu mazingira kwenye chanzo hicho, wanachangia kupungua kwa maji kwa kuwa ng'ombe mmoja kwa siku anakunywa wastani wa lita 45, hivyo kwa ujumla wao, wanakunywa lita 225,000.

Kutokana na hali hiyo, alimwagiza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, kuchukua hatua za haraka kudhibiti mifugo katika mito yote nchini, Ruvu ukiwamo ili kupunguza athari za ukosefu wa maji na uharibifu wa mazingira.

Kauli hiyo ya Rais imetoa mwanga ni namna gani uharibifu wa mazingira ulivyokithiri kutokana na shughuli za kibinadamu kwenye mito ambayo ni tegemeo kwa ajili ya uhai wa Watanzania.

Kwa muda mrefu tumeshuhudia shughuli za kibinadamu zikiwamo kilimo na ufugaji, zinavyoharibu mazingira na vyanzo vya maji na matokeo yake kuweka rehani maisha ya watu kwa kukosa maji.

Awali, ilielezwa kwamba kina katika Mto Ruvu kinapungua kwa sababu baadhi ya wawekezaji wamechepusha maji kwa ajili ya shughuli zao lakini hili la mifugo limeleta mshtuko zaidi.

Kutokana na taarifa ya Rais kwamba mifugo hiyo kwa siku inakunywa lita 225,000 ina maana kwamba kwa wiki inatumia lita 1,575,000 na kwa mwezi lita milioni 6.3, jambo la kujiuliza kwa mwaka ni lita ngapi za maji zinazopotea kutokana na idadi hiyo ya ng'ombe ambao pia wanazaliana?.

Licha ya matumizi ya maji, ni kiwango gani cha uchafuzi wa mazingira kinafanyika?

Hali hiyo inaonyesha dhahiri kwamba kuna athari kubwa zinazotokana na uharibifu wa vyanzo vya maji kwa sababu ya shughuli za kibinadamu kama ambavyo imekuwa ikielezwa mara kwa mara.


Mwaka 2006 wakati wa serikali ya awamu ya nne, uamuzi mgumu ulichukuliwa wa kuondoa mifugo katika bonde la Ihefu ambalo ni chanzo muhimu cha upatikanaji wa maji hususan mto Ruaha, hivyo hatua hizo pia zinapaswa kuchukuliwa katika mito yote na kwenye vyanzo vya maji. Kama alivyosema Rais juzi, kuna uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanyika sasa katika maeneo mbalimbali, hivyo hatua zinapaswa kuchukuliwa haraka.

Kwa mantiki hiyo, agizo la Rais Samia juu ya uondoshaji mifugo katika Mto Ruvu na mingineyo, halina budi kutekelezwa haraka ili kunusuru madhara yanayoweza kujitokeza siku zijazo.

Waziri Ndaki na timu yake wanapaswa kuhakikisha wanafanya haraka kutekeleza agizo hilo na haitarajiwi kukawepo siasa au kulegalega. Kama wahenga wasemavyo sheria ni msumeno, watu hao waliovamia vyanzo vya maji hawatakiwi kuonewa haya kwa sababu kuendelea kuwapo kwao ni maafa kwa mamilioni ya Watanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Kero hizi za mabasi kituo cha Msamvu zitafutiwe ufumbuzi

**KITUO** cha mabasi cha Msamvu mjini Morogoro, ni miongoni mwa vituo vya kisasa ambacho kinapokea mabasi kutokea mikoa mbalimbali nchini, kipo karibu na makutano ya barabara za kwenda Iringa na Dodoma.

Pamoja na ubora wake unaopambwa na majengo mazuri yanayokizunguka, kimekuwa pia kikikabiliwa na kasoro kadhaa, ambazo wakati mwingine ni kero kwa abiria na watu wengine wanaofika kupata huduma mbalimbali.

Ni mwanzoni mwa mwaka huu, lilitukia tukio la mpigadebe kumuua mwenzake wakati wakigombea abiria, hali ambayo ilisababisha taharuki kituoni hapo kutokana na mauaji hayo.

Tukio hilo lilisababisha kituo hicho kuwa na dosari ambayo ni muhimu sasa serikali ya mkoa na wadau wengine kwa ujumla, kuhakikisha hakuna mpigadebe anayeingia na silaha kituoni hapo tena.

Nimegusia kidogo tukio hilo, lakini lengo ni kutaka kuelezea kero ambayo baadhi ya abiria wamekuwa wakikumbana nayo wanapofika kituoni hapo kutafuta usafiri wa kwenda maeneo mbalimbali nchini.

Yako baadhi ya mabasi ambayo husababisha usumbufu kwa abiria, kutokana na mtindo wa madereva na makondakta kuweka wapigadebe ndani kwa lengo la kuwafanya abiria waamini kuwa yanakabiria kujaa ili yaondoke. Udanganyifu huo unawapata abiria wenye haraka ambao hukata tiketi wakiwa ndani ya mabasi hayo wakiamini yana muda mfupi ili yaanze safari na kumbe waliomo ndani, wengi wao si abiria bali ni wapigadebe.

Mazingira kama hayo, kwa abiria mwenye haraka ya kutaka kuwahi kule anakokwenda ni kero, hivyo ingekuwa ni vyema wakaacha mtindo huo wa kudanganya, badala yake wawaambie ukweli ili waamue kupanda au waache.

Inakera kuambiwa kuwa basi linakaribia kujaa liondoke na kumbe waliomo ndani wamewekwa ili kuvutia mtu akate tiketi, akifanya hivyo, wanashuka mmoja baada ya mwingine kadri abiria wanavyoongezeka.

Kwenye usafiri wapo baadhi ya abiria huwa wana haraka zao, hulazimika kukatia tiketi kwenye basi, sasa wanapokutana na udanganyifu kama huo wakati wameshakata tiketi, hujikuta ratiba zao za safari zikiharibika.

Wakati hao wakifanya mchezo huo, wapo madereva wengine ambao hutoa mabasi ndani ya kituo wakidai kwamba wanaondoka, kumbe wanakwenda kuegesha nje na kuanza kusubiri abiria huko hadi yajae.

Mbinu hizo mbili wanazotumia, kimsingi ni usumbufu kwa abiria wenye haraka na pia wanajikosesha uaminifu, hivyo ingependeza kama watakuwa wanafuata ratiba za safari, badala ya kutafuta abiria kwa kuwadanganya.

Labda niwakumbushe tu kwamba, katika ulimwengu wa biashara, uaminifu umekuwa ni kitu muhimu kuliko vitu vingine vyote vilivyowahi kutokea vinavyochochea mafanikio kwenye biashara.

Neno uaminifu si geni masikioni mwetu. Ni neno linalogusa kila mahali katika mzunguko wa maisha ya mwanadamu. Uaminifu unatakiwa kote kuanzia mahusiano, biashara uongozi, ndoa, masomo na katika kazi.

Uaminifu ni imani ambayo mtu anakuwa nayo kwa mwingine juu ya jambo fulani, lakini pia haishii kwa mtu na mtu tu, bali inakwenda mbali zaidi, inaweza kuwa kati ya taasisi na mtu, mtu na taasisi ama taasisi kwa taasisi.

Hivyo, ni vyema madereva na makondakta wanaofanya mchezo wa kuwadanganya abiria wakatambua kuwa uaminifu ni muhimu katika nyanja zote na unasaidia kuboresha huduma ya usafiri iwapo watautumia vizuri.

Ni vyema wakafikiria uwajibikaji wao, wanatumia muda gani kutekeleza majukumu, ahadi zao, lakini pia wajue kuwa mwisho wa siku wanajisikiaje wanapowadanganya abiria ambao kimsingi ndio wateja wao wakuu.

Si vibaya hata mabosi wao wakawajengea uwezo wa kile wanachokifanya, ili kiwe na matokeo mazuri badala ya kuacha malalamiko kwa abiria, kitendo ambacho kinaweza kusababisha wakose wateja.

Kwa kawaida watu wanataka kukuamini wakiwa na uhakika kwamba wanachoamini ni kweli, lakini wanapokutana na usanii kama huo wa abiria kudanganywa, wanakuwa wanajiweka katika mazingira ya kutoaminika.

Maadili mema na tabia njema ni muhimu kama kweli wanataka kujenga uaminifu kati yao na wateja wao, katika biashara ya usafirishaji abiria.

Hivyo, ni vyema kujenga tabia ya kuwa wakweli na wanyenyekevu kwa wateja wao.

## FIKRA MBADALA

# Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu



Pascal Mayalla

BAADA ya kuwapo nchini Burundi kwa wiki kadhaa, baada ya kushauriwa na kiongozi wetu mmoja, sasa nimerejea nchini kwa muda, kisha nitarejea huko. Kwa vile mimi ni mwanahabari, safari ijayo nitaanzia jijini Kampala, Uganda, kuwaletea ya huko.

Niliporejea nchini nimepokewa na Wiki ya Huduma kwa Wateja ya kampuni ya mafuta ya TotalEnergies. Kuna msemo wa Kiswahili usemao umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu" wenye lengo la kusisitiza ushirikiano na wengine. Hata kwenye kutembea na kukimbia au kufanya mazoezi, kuna msemo usemao ukitaka kwenda haraka, tembea peke yako au kimbia peke yako.

Kweli utatembea haraka na kukimbia lakini hutafika mbali, utachoka mapema na utaishia njiani. Lakini ukitaka kufika mbali, tembea na wenzio au kimbia na wenzio.

Sisi Tanzania katika dhana ya kushirikiana, kuna mahali tunakwama na majirani zetu wanatupita. Natolea mfano wa mchezo wa riadha, kwenye eneo la bara lote la Afrika, Tanzania ndio tunaongoza kwa kuwa na milima mirefu na safu nyingi za milima, tukiongozwa na Mlima Kilimanjaro, Mlima Meru, Safu ya Milima ya Usambara, tuna Kitonga.

Wenzetu Kenya, wao wana Mlima Kenya, Uganda wana Rwenzori na Ethiopia wana Safu ya Abysinia. Watu wa makabila ya milimani, wawindaji na wafugaji ni wakimbiaji hodari.

Miaka ya 1970, Watanzania ndio tuliongoza kwa riadha duniani. Tulitoa wanariadha mashuhuri kadhaa kama Filbert Bayi, Selemani Nyambui, Juma Ikangaa na Gidamis Shahanga ambao kila mmoja alikimbia mwenyewe na kushinda. Wenzetu Kenya na Ethiopia nao wakaanza ila wao badala ya kuacha mkimbiaji mmoja mmoja, waliwatafuta wakimbiaji wengi na kuwaweka pamoja na kutokana na wingi wa wakimbiaji, Watanzania tukaanza kupitwa. Mwishowe tumeachwa kabisa kuwika kwenye riadha!

Mbinu inayotumiwa na Wakenya ni baada ya kumjua mkimbiaji wake fulani ni mzuri, anawekewa wasindikizaji wa kumtia moyo, wanaoitwa "pace makers" na akifika raundi ya mwisho, anachomoka kama mshale! Wakimbiaji wa Tanzania, wanakimbia wenyewe, hakuna mtu wa kuwasindikiza, hivyo wanaanza mbio na kuishia katikati kwa kuchoka na kupitwa.

Sasa hii kampuni ya mafuta ya TotalEnergies Marketing Tanzania Limited kwa kuujua umuhimu wa umoja ni nguvu, katika kuadhimisha msimu wa nne wa Wiki ya Huduma kwa Wateja katika kituo cha mafuta cha TotalEnergies Bagamoyo Rd, Morocco, yenye kaulimbiu ya "Pamoja kila hatua" wameunganisha nguvu na kuanza ushirikiano mpya na Royal Oven Bakery.

Ukifika katika kituo cha mafuta cha TotalEnergies, utakutana na One Stop Shop, ambapo sasa ukifika vituo vya mafuta vya TotalEnergies, hutaishia kupata tu huduma za kuuziwa mafuta, bali kila kituo kina duka la Cafe Bonjou ambalo linauza mahitaji mbalimbali ya nyumbani, na sasa pia utakutana na Royal Oven food concept katika Kituo cha TotalEnergies cha Barabara ya Bagamoyo eneo la Morocco ambacho kinatoa huduma za chakula, "fast food" .

Kwa wiki hii nzima wametoa ofa ya baga ya nyama ya ng'ombe. Ukinunua moja, unapata nyingine bure.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa TotalEnergies Marketing Tanzania Limited, Jean Francois Schoepp, alisema: "Wateja ndio chachu ya biashara yetu na chachu ya mabadiliko, ukuaji na ubunifu wetu ili kuhakikisha kuwa tunaendelea kukidhi na kuvuka mahitaji na matarajio yao kwenye huduma za TotalEnergies. Wiki hii tunawaalika wateja wetu, kufurahia huduma bora kutoka kwa maofisa wa TotalEnergies, kufahamu matangazo mbalimbali yatakayoendeshwa katika vituo vyetu na kushiriki nasi maoni kuhusu bidhaa na huduma zetu."

Aliongeza kuwa katika TotalEnergies wanaamini kuwa Wiki ya Huduma kwa Wateja ni zaidi ya kusherehekea wateja lakini pia kuwa na ubadilishanaji wa maana na kupokea maoni. Kwa hili, alisema wanawahimiza wateja kutumia mifumo ya mtandaoni ambayo itawasilishwa katika vituo wiki hii na kutumia maoni ambayo watafurahi kuyapitia yote na kuboresha bidhaa na huduma zetu kwa kuridhika kwako.

Pia wanawaalika wateja kufurahia ofa na promosheni mbalimbali zinazopatikana katika vituo vyao na kupata nafasi ya kujishindia zawadi kadhaa zikiwemo burger ya nyama ya ng'ombe, fulana, kofia, pete za funguo na huduma za bure za kubadilisha mafuta"

Kutokana na uzinduzi wa ushirikiano kati ya TotalEnergies Marketing Tanzania Limited na Royal Oven Bakery, Meneja Mkuu wa Royal Oven Bakery, Patrick Meme, alisema kampuni yake ina furaha kubwa kushirikiana na TotalEnergies na kuwa sehemu ya dhana yake ya kituo kimoja ambapo itakuwa ikiwapa wateja maandazi mapya, baga, pizza, keki na mengine mengi kila siku kuanzia saa 12 asubuhi hadi 4 usiku.

Mkurugenzi wa Masuala ya Sheria na Uhusiano, Getrude Mpangile, anawaalika wananchi kujitokeza kwa wingi kwenye vituo vya Total katika vituo vya TotalEnergies katika wiki hii ili kupata zawadi mbalimbali na huduma za ziada, si tu kwamba utapata mafuta na vilainishi vya hali ya juu vilivyoongezwa kiambata cha 'execillium', pia bidhaa za matumizi ya kawaida zenye ubora wa hali ya juu.

Ama kweli umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Kama kampuni kubwa kama TotalEnergies inafanya ushirikiano na wengine, vipi kuhusu vikampuni vidogo vidogo? Ukitaka kufika mbali, shirikiana na wengine.

**Wasalaam.**
**Paskali**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tumempenda Jackson Majaliwa nyie msimpende sana!



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

WATANZANIA bado tuna kiwewe na maumivu yaliyosababishwa na ajali ya ndege ya PrecisionAir katika mwalo wa Bukoba, ziwani Victoria ambapo ndugu zetu 19 walitangulia mbele za haki na kuwaacha wengine 26 wakiugulia maumivu.

Pamoja na hali hiyo, bado tunaendelea kumwombea kijana wetu shujaa ambaye hakutarajiwa, Jackson Majaliwa, aliyejitosa ziwani na kuweka rehani maisha yake, ili mradi tu aokoe roho za Watanzania wenzake ambao hata si wa familia au ukoo wake.

Sambamba na hilo, wapo watu wengine ambao nao wanatumia tukio hilo kama kiki ya kujitafutia umaarufu hasa kuelekea mwaka wetu mashuhuri wa uchaguzi. Lakini hiyo isiwe taabu, wacha wapate kiki lakini kama wanasaidia, basi Mungu awarudishie walikopunguza.

Shujaa Majaliwa, amezidi watu wengi kwa moyo wake wa kuokoa roho za watu, na kama isingekuwa kuingiliwa na kuzuiwa na waliojifanya kujua zaidi, bila shaka zile roho zingine 19 nazo zingeokoka na tungekuwa nao hivi sasa.

Majaliwa, ambaye bila shaka ipo siku atapewa Tuzo kubwa na ya heshima, kwa kazi hii aliyoifanya mbali na kupewa ajira na kiasi fulani cha kifuta jasho, hakika amezidi hata baadhi ya wachungaji ambao kila kukicha hupiga kelele za "Toka! Toka! Shindwa na ulegee!" Huku wakikomba pesa za watu kwa jina la sadaka.

Wakati Majaliwa alijitoa muhanga kujitosa majini kuokoa watu tena bila kudai ujira, wachungaji hao wamekuwa wakiweka mpaka viwango vya sadaka ili kuwakamua wanaowaita waumini wao, huku wakiwadanganya kuwapeleka Mbinguni na wengine kuwafufulia wafu wao, lakini mwishowe ni utapeli mtupu.

Kama utajiri wanaopata baadhi ya wachungaji hao umekuwa kweli unatoka kwa Mungu, bila shaka leo hii kufumba na kufumbua Majaliwa angekuwa na mahekalu na magari kedekede ya kifahari na miakaunti ya pesa katika kila benki kutokana na alichokifanya.

Hakika kwa roho alizookoa, bila shaka huyu ndiye anastahili uchungaji wa kweli na nasema mpaka sasa kwa kazi aliyoifanya, ukichukulia uzito wake, basi haujalingana na kazi aliyopewa sasa, ingawa Serikali kupitia kwa Chifu Hangaya inapaswa kushukuriwa kwa hata hicho kidogo alichotunukiwa Majaliwa.

Lakini bado imetufunza, kuwa tusikae tunabweteka katika mambo yetu ya kila siku, tukisubiri majanga yatukute huku tumelala usingizi wa pono na matokeo yake kubaki tukipigwa butwaa kutokana na vijana wadogo wa miaka 20 kama Majaliwa, tena wavuvi wa dagaa, kutuzidi fikra na kuamua haraka kama alivyofanya.

Binafsi napongeza alivyotambuliwa na alichopewa, lakini bado sijaridhika, kwani Majaliwa alitakiwa aachwe alikokuwa na aendelezwe akiwa pale pale, badala ya kumpeleka kwenye ajira katika kikosi cha uokoaji na zimamoto, kwa sababu huko hatakuwa na kipato cha kumridhisha.

Kama mathalan angewezeshwa katika uvuvi wake kwa kupewa zana za kisasa na mtaji wa kutosha, bilashaka, kwanza angebaki eneo la majini aliko na ujuzi nako, na endapo kungetokea la kutokea, angekuwa tayari kukabiliana nalo, lakini pia angejiongeza kipato na kuisaidia familia yake, ambayo bila shaka ni duni kiuchumi.

Sikosoi kilichofanyika, hapana, yawezekana Chifu Hangaya kama alivyo mtu wa malezi, Mama anayependa watu wake, pengine aliona kama Majaliwa huko aliko anateseka, hivyo akiwa Zimamoto atafanya makubwa binafsi na kwa Taifa, ndipo akaamua haraka haraka kumpa nafasi hiyo.

Lakini kwa hali ilivyo, bila shaka Majaliwa akishamaliza masomo yake akaanza kazi, hatakuwa wa ajabu, kwa sababu hatuishi kwa majanga na inawezekana kabisa akaja kuwa mtu wa kawaida tu na asiyefuatilia majanga kama ilivyo sasa, akiambukizwa na wengine ambao si kama yeye na ndiyo sababu hata siku ya siku hawakuwahi kwenye tukio.

Lakini pia, tuelewe Majaliwa ana elimu ya kidato cha pili tu, alishindwa kuendelea na masomo kutokana na uduni wa maisha ya familia yake, na hivyo kuamua kuingia majini kutafuta japo kitu cha kula yeye na familia yake na ndipo akaja kujulikana kwa ajali ya ndege, kwa bahati mbaya tu.

Najiuliza, je huko baadaye akija mtu mwingine wa kutuongoza akasema wale wasio na vyeti vya kidato cha nne waondoke, Majaliwa atasalimika kweli? Kwa nchi hii si ajabu! Tujiulize ilikotoka amri ya walioghushi vyeti waondoke! Na kama si Chifu Hangaya hata hiyo michango yao kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii wasingeambulia. Hebu tubungue bongo kidogo kuhusu mustakabali mwema wa mkombozi wetu, Jackson Majaliwa.

**Alamsiki!**

# Wananchi waiangukia serikali kutowahamisha

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

ZAIDI ya wananchi 20,000 ambao ni wakulima wa mpunga katika vijiji vitano vilivyopo Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameiangukia serikali na kuiomba iwape nafasi nyingine ya kuwasikiliza kabla ya kuwahamisha katika maeneo ya hifadhi ambayo imeonekana wameyavamia.

Wananchi hao wameomba kupewa nafasi hiyo ikiwa ni wiki chache tangu kamati ya mawaziri wanane wa kisekta ifike wilayani hapa na kuagiza wakazi wa vijiji vya Luhanga, Iyala, Madundasi, Msanga, Kilambo na vitongoji zaidi ya 40 kuondoka mara moja katika maeneo hayo kupisha eneo la hifadhi.

Wakizungumza na Nipashe juzi, wananchi hao walisema wanatamani kupata nafasi nyingine ya kutoa hoja zao ili serikali izisikie na kuzipima zaidi kabla ya kuwaondoa.

Abulkarim Mwanginonya, alisema wako tayari kushirikiana na serikali lakini kabla ya utekelezaji wa hatua hiyo wanaomba kusikilizwa zaidi.

"Tunafahamu viongozi walikuja hapa na kufanya mkutano, lakini tunaomba waje watusikilize tena kwa sababu tunaona wakati wamekuja kufanya mkutano muda ulikuwa finyu, kwa hiyo tunaomba watenge siku nzima waje watusikilize hoja zetu ambazo tunaamini huenda zikasaidia kwenye jambo hili," alisema.

Mwaingonya alisema wakazi wengi katika vijiji hivyo wamewekeza kwa kiwango kikubwa katika kilimo, hivyo ni vyema serikali ikaangalia namna ya kuepusha hasara zitakazowapata endapo wataondolewa bila kuwasikiliza.

"Unapofuta vijiji hivi, sisi tunakwenda kufanya nini wakati shughuli zetu ni kilimo na zinategemea hili bonde? Kutuondoa bila kusikiliza hizi hoja tunazotamani zisikilizwe tutateseka sana," alilalamika.

Upendo Kyambiki, mkazi mwingine wa eneo hilo, alisema wanaamini kilio chao kitamfikia Rais Samia Suluhu Hassan na atawasaidia.

"Tunamwomba Rais wetu asikilize haya tunayoyaomba na tunaamini atatusaidia katika hili kwa kuwa ametatua mengi ya namna hii, hatuna sehemu ya kupeleka watoto wetu," Upendo alisema.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, aliiambia Nipashe juzi kuwa maeneo ya vijiji na vitongoji hivyo yako kwenye eneo la hifadhi na serikali ilifanya makosa kusajili vijiji hivyo.

Dk. Mabula alisema serikali inaandaa utaratibu wa kuwapangia maeneo mengine wananchi hao ambako wakwenda kuendesha shughuli zao.

# RC aipa mbinu EWURA kuimarisha utendaji wake

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

MKUU wa Mko wa Iringa ameitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuendelea kushughulikia maslahi ya wafanyakazi kwa wakati ili kuimarisha utendaji kwa taasisi hiyo.

Halima Dendego alitoa rai hiyo jana alipofungua kikao cha nne cha Baraza la Wafanyakazi wa EWURA lililofanyika mjini hapa. Alisema maslahi ya wafanyakazi yakishughulikiwa kwa wakati, yataondoa malalamiko sehemu za kazi na kuchochea ufanisi.

"Ni muhimu menejimenti kuwa karibu na wafanyakazi wenu, shughulikieni maslahi yao kwa wakati ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima," alishauri.

Mkuu huyo pia aliwataka wafanyakazi wa EWURA kuwa na staha wanapodai maslahi yao na kuwajibika katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

AliIshukuru mamlaka hiyo kwa kutoa Sh. milioni 10 kwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Iringa kusaidia ujenzi wa uzio na Sh. milioni 10 kuunga mkono juhudi za kuimarisha utalii kwa nyanda za juu kusini katika kushamirisha tamasha la Utalii Karibu Kusini 2022.

Akizungumzia msaada huo, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA Modeatus Lumato, alisema mamlaka imekuwa na utaratibu wa kusaidia jamii katika nyanja mbalimbali na kipindi hiki imetoa kipaumele katika eneo la elimu na utalii.

"Sisi EWURA tumeona ni vyema tusaidie kuimarisha miundombinu ya elimu pamoja na kuhamasisha utalii wa ndani kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan katika masuala hayo," alisema.

Mwakilishi wa Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Iringa, Mikodadi Rashid alisema msaada huo utakuwa chachu ya kuboresha mazingira ya kusomea. Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa TUGHE Taifa, Amani Msuya aliagiza taasisi zote za umma kuhakikisha zinakuwa na utaratibu wa kuimarisha maslahi na hali bora za wafanyakazi.



Wateja wakinunua embe katika eneo la Kitunda jijini Dar es Salaam jana ambapo fungu moja linauzwa kwa shilingi 1000. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NMB yajivunia kwa uwezeshaji wanawake

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BENKI ya NMB imetaja akaunti yake ya Fanikiwa kuwezesha wanawake wengi kujiimarisha kiuchumi na kuongeza mitaji jambo lililowavutia wengi hasa walioko vijijini.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Shughuli za Serikali wa Benki ya NMB, Vicky Bishubwa alipozungumza na mamia ya wananchi waliojitokeza kwenye uzinduzi wa kitabu cha Continuity With Vision The Roadmap to Success for President Samia Sukuhu Hassan.

Benki ya NMB ilikuwa miongoni mwa waliofanikisha shughuli za utambulisho na uzinduzi wa kitabu hicho kinachomhusu Rais Samia Suluhu Hassan hasa katika utendaji kazi wake ndani ya serikali.

Bishubwa alisema tangu walipotambulisha Fanikisha Akaunti, imepata mwitikio mkubwa kwa kuwa wanawake wengi, hasa wafanyabiashara ndogo wamekuwa wakikimbilia huko baada ya kuona masharti yake ni rahisi na fedha za mkopo zinatoka kwa haraka huku riba ikiwa ndogo pia. "Kwa muda mfupi tumetoa mikopo 9,265 yenye thamani ya karibu Sh. 30 bilioni kwa wanawake wajasiriamali. Kwa hiyo tunaposema NMB Karibu Yako, hii ndiyo maana halisi," alisema Bishugwa. Mbali na akaunti hiyo, ofisa huyo alisema kwa sasa wamekuja na mpango wa NMB Asili ambalo ni jukwaa la kuwawezesha kinamama kufikia ndoto zao ndani na nje ya nchi huku kipaumbele zaidi kikiwekwa kwa wanawake wa vijijini.

Katika kuonyesha mwitikio ni mkubwa kwa benki hiyo, alisema mwezi April mwaka huu waliweka malengo hati fungani katika soko la Hisa la Dar es Salaam na kuweka lengo la kukusanya Sh. bilioni 25 lakini mwitikio ulipelekea wakakusanya karibu Sh. bilioni 75 ambayo ni asilimia 300 ya lengo.

Akizungumza kuhusu kitabu hicho, mwakilishi huyo wa Mtendaji Mkuu wa NMB, alisema wataendelea kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali na wasomi kwa namna yoyote inayogusa maisha na maslahi ya Watanzania wanyonge.

Akizindua kitabu hicho kwa niaba ya Waziri Mkuu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda aliwashukuru Eastern and Southern African Universities Research Programme (ESAURP) ambao waliwezesha kutungwa kwa kitabu hicho kilichobeba sura ya Tanzania kwa maisha ya kiongozi wao.

Prof. Mkenda alisema kitabu hicho chenye kurasa 624, kimeandikwa na wasomi na wanazuoni 45 na kuhaririwa na wasomi wa juu miongoni mwao ni Prof. Ted Maliyamkono na Prof. Provident Dimoso wa Chuo cha Mipango. Waziri huyo alishukuru taasisi zilizowezesha kusanyiko hilo ikiwamo Benki ya NMB na kuwataka wasiishie hapo tu kwa kuwa serikali inawategemea katika mambo mengi ikiwamo kuwawezesha wananchi wake kiuchumi.

Alisisitiza wananchi kusoma vitabu ili kujenga uelewa kwa kuwa Tanzania inahitaji kufanya mageuzi makubwa katika elimu, hivyo baadhi ya watu wanaweza kujikuta wanaachwa nyuma kama hawatakuwa na juhudi za kujisomea na kudadisi.

# MAISHA

NOVEMBA 13, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


## Furahia mishkaki

Yajue haya kabla ya kuanza ujenzi wa nyumba



## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# KUWA 'HANDSOME'

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | J | E | M | B | E |
| | A | | | O | |
| U | M | A | | N | |
| | B | | I | G | A |
| | I | | | E | |
| J | A | N | G | A | |

## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
DAU, AMA, TAMBI, JAZWA, WAKATI, JAMBIA

## TOA TOFAUTI 5






## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MAZUNGUMZO ya marafiki wawili walipokutana mara walipomaliza kipindi cha somo la Jiografia darasani.

Juma: Mwalimu kasema eti volcano inatoka chini ya ardhi, jambo hili linanishangaza.

John: John kwa nini unashangaa, unaambiwa ikitoka inakuwa kama moto.

Juma: Sasa huko chini moto utawakaje na kawasha nani?

John: Umejitengeneza wenyewe

Juma: Sasa utawakaje wakati hakuna hewa ya oksijeni, au na huko kupo kama huku kwetu.

Alichokifanya Adaktari

Swali

Mlima Kilimanjaro unashika nafasi ya ngapi kwa urefu Afrika?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Natamani kujua ndugu zangu, baba alinificha

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vimbwanga vya Maisha Ndivyo Yalivyo. Wakati tunapoelekea ukingoni mwa mwaka huu wa 2022, wapo watu wengi wanajiuliza maswali ni kwa nini wapo hapo walipo pasipo mafanikio au hawafurahii maisha?

Kitu ambacho wengi wetu hatuelewi ni kwa jinsi gani ya kufanya vitu vilivyoko kwenye ulimwengu wa roho ili vidhihirike kwenye ulimwengu wa damu na nyama. Yaani ulimwengu huu tunaouona kwa macho yetu ya kimwili.

Ulimwengu wa roho (ule usioonekana), ndio unaotawala ulimwengu wa mwili (unaoonekana). Huko hufanyika vitu pasipokuonekana, kisha vikadhihirika katika macho ya kimwili.

Yapo mambo ambayo hufanyika kwa siri lakini baadaye yanakuja kufahamika, na matokeo yake kuleta madhara au maumivu makubwa kwa wahusika.

Kwa mfano, baba aliyeko kwenye ndoa, akavutiwa na mwanamke nje ya ndoa na akazaa mtoto. Mara nyingi mtoto wa aina hii hujikuta kwenye msukosuko hasa anapotafuta kutambuliwa na familia ya baba yake!

Hivi karibuni nilimtembelea mama mmoja rafiki yangu kumjulia hali. Wakati tunazungumza, akapokea simu toka kwa ndugu yake aliyeko ng'ambo(ulaya). Nilichonasa kwenye maongezi yale kijana akamuuliza dada yake, je, hapo ulipo upo peke yako tuongee? Akajibiwa kuwa huru nipo mwenyewe.

Kijana akamuuliza kama alishatoa taarifa kwa ndugu kwamba anahitaji kutambuliwa kwenye familia na ukoo wa baba yake. Dada akamwambia bado, kwani wanatafuta namna ya kumweleza na kumshawishi mama mlezi wa familia ya baba amkubali kwani baba alishafariki. Hata hivyo, dada huyu alimwambia kuwa bado anafuatilia jambo hilo kupatia ufumbuzi. Baada ya mazungumzo hayo ya simu, ikabidi nipate maelezo zaidi kuhusu jambo hilo. Mama huyu rafiki yangu akasema kuwa ni kweli baba yao alimzaa kijana huyo nje ya ndoa, akamsomesha.

Akasema ni msomi mzuri, ana kazi nzuri ulaya, lakini anatamani sana kutambuliwa kwenye familia ya baba yao. Akasema upo wakati aliambiwa aje nyumbani wakati baba mzazi akiwa hai hakuweza kuja. "Angekuja wakati ule ingekuwa rahisi kwani baba angemtambulisha mwenyewe, lakini sasa inakuwa ngumu".

Mpenzi msomaji, ona jinsi kijana huyu anavyotaabika kutafuta kuwajua ndugu zake. Siyo kwamba anataka urithi kwani mali anazo, ila utambulisho tu! (Maombolezo 5:7) Neno la Mungu linasema,"Baba zetu walitenda dhambi, hata hawako; na sisi tumeyachukua maovu yao".

Maovu ya baba yake aliyechepuka na kumzaa kijana huyu nje ya ndoa, ndiyo yanayomtesa hivi sasa. Anajiona yuko peke yake, lakini kiuhalisia anao ndugu zake ambao baba yake hakutaka kumtambulisha kwake mapema.

Yapo mambo mengi yanafichwa ikidhaniwa kuwa hayajulikani, na hata kama yakigundulika eti hayana madhara, kumbe huko ni kujidanganya. Hata wahenga walisema, "mficha maradhi, kifo kitamuumbua. Kama ulimzaa kwa raha zako, kwanini leo unamkataa na kuficha hiyo siri?. Ni dhahiri wapo watu wengi wanakumbana na kadhia kama hii. Walificha watoto waliowazaa nje ya ndoa na kwa sababu hawakutambulishwa wakajikuta wanaoana ndugu kwa ndugu. Mifano ipo, nitakumegea kisa Jumapili ijayo. Wachumba wanafikia hatua ya kufunga ndoa, kumbe ni ndugu hawapaswi kuoana!

Utafiti kuhusu kadhia hii ya watoto nje ya ndoa, unaonyesha kuwa wengi wamekuwa ni wenye vipaji vikubwa, wenye kazi nzuri zenye mafanikio kuliko hata wale wanaozaliwa ndani ya ndoa.

Yupo dada mmoja alizaa na mume wa mwanamke mwenzake. Mtoto huyo wa kiume alipofikisha umri miaka minne mama akafariki. Baba akampeleka kwa dada yake amtunze huku akitoa huduma zote.

Kijana alipofikia sekondari baba akawa na uthubutu kumtambulisha kwenye familia. Ijapokuwa mama alileta upinzani lakini baadaye ilibidi awe tu mpole. Baba alikuwa mfanyabiashara, akamshirikisha kijana kwenye miradi yake.

Alifanya hivyo hata kwa watoto wakubwa wa mke wake. Cha ajabu kijana huyu nje ya ndoa alifanya vizuri katika miradi kuliko wale ndugu zake wawili.

Hao walikuwa walevi, viburi, wapenda anasa hivyo badala ya kuzalisha faida, wao walisababisha hasara kwa kampuni.

Hata hivyo, kinababa wengi hujikausha, hupotezea watoto nje ya ndoa kuokoa ndoa zao. Zipo zilizobomoka kwa tatizo hilo. Wakati mwingine ni bora kukubali matokeo, yaishe.

Hadi wiki ijayo. Una kisa? **Ujumbe. 0715268581 .**

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Kilio cha marubani kuhusu ubora wa ndege kisikilizwe

MWISHONI mwa wiki iliyopita Chama cha Marubani Tanzania (TAPA), kilipaza sauti kuhusu matatizo mengi yaliyoko kwenye tasnia ya usafiri wa anga ambayo yanapuuzwa na wasafirishaji na mamlaka za serikali.

Rubani ambaye hakutaka kutajwa jina lake, alisema Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), imepuuza malalamiko na maonyo wanayotoa kuhusu usalama wa ndege. Alisema wamewahi kujikuta wakilazimishwa kurusha ndege hata katika mazingira yasiyoruhusu.

Alikwenda mbali zaidi kwa kueleza kuwa kuna marubani waliteswa sana siku za nyuma kwa kuwa walikataa kurusha ndege kwa sababu za msingi kabisa wakaambiwa "sisi ni shirika la miaka mingi, rusha ndege kwa kuwa watu wako uwanja wa ndege na wamekata tiketi."

Aidha, alisema hata walivyopeleka ripoti TCAA kuwa wamekataa kurusha ndege kwa sababu ya hatari hawakusikilizwa, zaidi waliishia kuchongewa kwa wamiliki wa ndege hali iliyowafanya wengi kukiuka miiko ya kazi zao kutokana na misukumo ya kiutendaji inayotokana na uamuzi wa watendaji wakuu.

Pia walisema waliwahi kumpelekea waziri mwenye dhamana lakini aliwaita TCAA na hakuna kilichofanyika huku wakidai wanaungana na wamiliki kuzima malalamiko ya msingi ambayo ni hatari kwa wasafiri.

Naye Kapteni Khalil Iqbal alisema kuna kamati ya usafiri wa anga ambayo wamekuwa wakipeleka siri za malalamiko yao kwa wamiliki wa ndege na kuziweka ajira zao shakani, huku akieleza wako waliofukuzwa kazi kwa kutoa taarifa kuhusu injini mbovu.

Haya yanaibuka baada ya ajali ya Kampuni ya Ndege ya Precision iliyoanguka Ziwa Victoria Novemba 6, mwaka huu, ikaua watu 19 na kujeruhi 26 (waliokuwa ndani ya ndege 24, wakiwamo marubani na wahudumu wawili).

Wataalam wa ndege wanadai matatizo ya usafiri huo yalionekana tangu Dar es Salaam ila kutokana na mwendelezo wa kuchukulia rahisi, safari iliendelea na mwisho ukawa mbaya.

Kwa sasa serikali na mamlaka zingine zinafanya uchunguzi juu ya mambo mengi yakiwamo madai kwamba kulikuwa na tatizo kabla ya safari na ndio maana wanatafuta kisanduku cheusi kinachohifadhi taarifa zote muhimu.

Ajali hii imetuacha uchi kama taifa juu ya uwezo wetu wa kukabili majanga licha ya kuwa na idara ya maafa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ina ofisi kila mkoa na wilaya ambako kuna kamati za maafa. Wananchi wa kawaida waliojifunza wenyewe ndio walifanya kazi kubwa ya kuokoa watu waliokuwa ndani ya ndege hiyo.

Walitumia akili zao za kuzaliwa na zana zao hafifu kuwaokoa watu 26 huku wakizuiwa kuokoa zaidi hali inayowafanya baadhi yao kufikiri kwamba wengi wangeokolewa kama wananchi wangeruhusiwa kufanya hivyo.

Kwa sasa ajali nyingi zinatokea hasa za barabarani watu wanakufa hata katika mazingira ambayo wangeokolewa na sasa kwa ajali ya ndege ambao ni usafiri unaoaminika ni salama duniani.

Mara kadhaa nimesafiri na ndege za mashirika mengi tofauti licha ya kwamba sina utaalam ila nimeshtuka sauti zisizo za kawaida zinazotoka hasa wakati wa kutua na kupaa wakati ambao ni wa hatari sana kwa usafiri wa anga.

Ajali hii itufundishe umuhimu wa kufanya matengenezo na uchunguzi wa kina si kwa usafiri wa anga pekee hata usafiri wa majini na barabarani ambao unaua mamia ya watu kila uchao.

Mathalani, kila siku yanaripotiwa matukio ya ajali za magari watu wanakufa, kujeruhiwa huku wengi wakibaki kuwa mzigo kwa familia zao ambazo ni maskini kwa kuwa fedha na mali zinatumika kumhudumia ndugu.

Bila kuchukua hatua kutafuta mzizi wa tatizo, kila siku tutapoteza nguvu kazi na kuacha mzigo mzito kwa familia. Wako watoto wamebaki yatima lakini kuna aliyebaki peke yake baada ya wazazi wake na wadogo zake kufa kwenye ajali.

Kwa ujumla, tusinyamaze na mamlaka za serikali ziwajibike ipasavyo kwamba idara ya maafa isiwe ni kwa ajili ya njaa au mafuriko bali kuwa na mbinu za uokoaji. Katika ajali ya ndege hadi saa saba mchana, siku ya tukio, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alisema bado wana mawasiliano na rubani lakini baadaye tunasikia naye ni mmoja wa watu waliokufa!

Kijana shujaa Jackson Majaliwa, anaeleza alijitahidi kuokoa wengi kwa kufungua mlango huku akitafuta kitu kizito apasue kioo kama alivyokuwa anaelekezwa na rubani lakini alikatazwa na viongozi wa uwanja wa ndege Bukoba.

Kwa hali ya ajali hizi maana yake hatuko salama, hivyo tunapaswa kutumia vyema akili na maarifa tuliyopewa na Mungu kwa sababu hata usafiri wa kundi la hali ya juu nao si salama kwao. Hii inatutaka tuchukue hatua na tuache kusema ni Mungu ameamua.




Ilikuwa furaha kwa ndugu na marafiki wa Gloria Samson baada ya kumfanyia sherehe ya kipekee ya kumuaga kwa ajili ya kwenda kuanza maisha mapya ya ndoa. Sherehe hiyo ilifanyika Oktoba 28 mwaka huu, katika ukumbi wa Cavilam barabara ya Iringa, Jijini Dodoma.











# MITINDO









# JIMWAGE NA VELVET

NENO "Velvet" lina maana ya "laini". Kwa hiyo vazi la velvet linapendwa kuvaliwa na wanawake kutokana na kuwa laini na mng'aro unaopendeza.

Kwa kawaida, kitambaa kinachoitwa Velvet kina sifa ya kuonekana laini na uzuri usio kifani.

Mara nyingi, kitambaa hiki hutumiwa kushona nguo za kifahari, lakini wakati mwingine velvet hutumiwa katika nguo za biashara.

Mwanzoni, velvet ilifanywa kwa vitambaa vya hariri na pekee nchini China. Baadaye, uzalishaji huu wa kitambaa ulijulikana katika HYPERLINK "https://uofa.ru/sw/teplye-strany-evropy-zimoi-gde-v-evrope-teplo-v-yanvare-luchshie-kurorty/" nchi za Ulaya. Kwa ajili ya utengenezaji wa velvet ilianza kutumia si hariri tu, lakini pia pamba, na baadaye nyuzi za bandia.

Wabunifu wa kisasa wameboresha kwa kutengeneza nguo za aina hiyo katika mitindo mbalimbali ya kuvutia.

Mara nyingi nguo za velvet hutumiwa katika shughuli za kijamiii kama harusi, hafla za usiku, burudani na kama nguo maalum za kutokea nyakati za jioni.

Mtindo wa kawaida

Bila shaka, mavazi haya huwezi kuyaona sehemu nyingi mitaani. Hii inatokana na hofu ya baadhi ya watu kwamba ni gharama kupata kitambaa chake, lakini ukweli ni kwamba kila mtu anaweza kuvaa kulingana na uwezo wake.

URAMBO

URENBO

URENBO


URENBO

URENBO

## UREMBO

**Na Mary Geofrey**

# KUWA 'HANDSOME'



WANAUME wengi wanasumbuliwa na tatizo la kuota upele baada ya kunyoa ndevu na kisha kuacha alama ya makovu na weusi mashavuni.

Kutokana na tatizo hilo kuwa kubwa, tutaelekeza namna ya kunyoa ndevu au sehemu nyingine za mwili bila kupata athari za upele.

Changamoto

Kupata vipele baada ya kunyoa hasa kwenye maeneo yanayozunguka kidevu, kwapani husababisha pia kuwashwa.

Inaelezwa kuwasha ngozi inasababishwa na ukavu unaoletwa na viua wadudu kama spiriti au bidhaa yenye pombe, kupata weusi unaotokana na kukauka kwa vipele vilivyopona baada ya kunyoa.

Changamoto hizi zinachangiwa zaidi na bidhaa na vifaa tunavyotumia kunyolea. Siyo wote wanapata vipele na weusi, ila kwa wale wenye tatizo hilo inachangiwa na vitu kadhaa.

Sababu zinazochangia tatizo

Kunyoa bila kulainisha ngozi, kupaka spiriti au aftershave yenye pombe, kutokupaka kitu chochote baada ya kunyoa na kutumia kiwembe kisicho na makali.

Namna ya kutibu tatizo

Lainisha ngozi kabla ya kunyoa kwa sababu ngozi ya juu ina chembe hai zilizokufa, ukilainisha ngozi kabla ya kunyoa itasaidia kuondoa na chembe hai zilizokufa wakati wa kunyoa.

Pia itasaidia wembe kuteleza vizuri kwenye ngozi bila kusababisha michubuko.

Tumia aftershave baada ya kunyoa ili kupoza ngozi, kuipa unyevu nyevu na kufanya kuwa nyororo.

Spiriti na aftershave zenye alcohol zinafanya ngozi kuwa kavu, itasababisha miwasho na ukijikuna ndiyo inapelekea kutoka vipele.

Nyoa kufuatisha muelekeo wa nywele zilivyoota, itasaidia ngozi isiume zaidi wakati wa kunyoa.

Hakikisha kiwembe unachotumia kunyolea ni kikali, kikiwa butu utarudia mara nyingi na kuumiza zaidi ngozi.

Usitumie deodoranti yenye chumvi ya aluminum na alcohol kwa sababu inachangia kufanya ngozi iwe kavu na kuwasha baada ya kunyoa na kupata weusi wa kwapa.



## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Furahia mishkaki

MISHKAKI inapendwa kuliwa na watu wengi, huwa mlo ambao hundaliwa maalum.

Watu hasa wanaume hupenda kula mishkaki mara nyingi wakiwa kwenye shughuli au sehemu za starahe.

Namna ya kutayarisha na kupika mishkaki ya nyama kwa njia iliyo bora na rahisi ni kama ifuatavyo.

**Mahitaji**

Nyama steki, ratili kilo mbili, mafuta vijiko vitatu vya supu na masala ya kulowekea nyama.

Mahitaji mengine ni kitunguu saumu, tangawizi iliyosagwa vijiko viwili vya supu, pilipili mbichi iliyosagwa kijiko kimoja cha supu.

Pia siki nyeupe vijiko vitatu, chumvi kiasi, cummin powder, ubizari masala,coriander powder, kijiko cha chai kimoja pilipili nyekundu ya unga na kijiko kimoja cha supu mdalasini wa unga na kijikokimoja cha chai.

**Kutayarisha na Kupika**

Kata nyama vipande vikubwa kiasi.

Changanya masala na vitu vyote katika nyama uloweke kwa muda wa saa mawili.

Tunga vipande vya nyama katika vijiti vya kuchomea mishikaki.

Choma katika jiko la makaa au katika B.B.Q kwa moto wa kiasi ukiwa unazigeuza geuza hadi nyama iive.

Epua, weka katika sahani ikiwa tayari kuliwa. Furahia mishkaki yako na ukitaka unaweza burudika na kinywaji baridi.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Yajue haya kabla ya kuanza ujenzi wa nyumba

## Namna ya kuchagua bomba ya pazia



DUNIA ya sasa inatawaliwa na uzuri na mambo yanayovutia ndiyo maana hata jinsi unavyofunga pazia unatakiwa kuwa makini ili kuifanya nyumba ipendeze zaidi.

Kwa hiyo unaponunua bomba za pazia zingatia haya.

1: Hakikisha unaweka mabomba ambayo yanaendana na mapambo mengine yaliyoko sehemu inakofung wa pazia husika.

2: Vifaa vilivyotumika kutengenezea bomba angalia imara kwani pazia japo hazina uzito mkubwa, lakini uimara unazingatiwa zaidi.

3: Hakikisha fimbo ni laini ya kuteleza kirahisi wakati wa kufungua na kufunga pazia siyo ngumu na kusa babisha kutumia nguvu kubwa.

Angalia matundu ya kwenye mapazia na unene wa bomba kama zinavalika bila kulazimisha.

Kumbuka kuangalia vifuniko vya mwisho vya bomba ambavyo navyo ni urembo.



UJENZI wa nyumba ni uwekezaji kama ulivyo uwekezaji mwingine wowote. Kwa maana hiyo , kuna maandalizi na mipango inayotakiwa wakati wa kufanya uwekezaji huo.

Ni vigumu sana kufanikiwa kuwa na nyumba ya ndoto yako endapo hujaweka mipango mizuri ya kuweka pesa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hiyo unayoitamani.

Mtaalamu wa ujenzi, Khamis Ally, anasema kuna vitu ambavyo mtu ambaye amekusudia kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba anapaswa kuvifahamu.

Moja ya vitu hivyo, anasema ni kuweka mipango madhubuti juu ya ujenzi wa nyumba katika mtazamo wa sasa na wa baadaye. Kwa maana hiyo, nyumba ambayo mtu anatakiwa kujenga ni ile ambayo itakuwa na sura na mvuto ambao utadumu kwa miaka mingi.

"Unapopanga kujenga nyumba yako ni muhimu kuiona baadaye na mabadiliko yake. Ni vyema ujue jengo lako litakavyokuwa kabla ya kuanza ujenzi, ufahamu uzuri wake, ukubwa, kimo, rangi.

"Ujue ni wapi utakwenda kununua saruji, mbao, nondo na vinginevyo, umfahamu fundi atakayekujengea, ukanda unaojenga ni wa aina gani kijiografia, ufahamu kama eneo lako halina mgogoro wowote iwe ni kwa upande wa serikali au majirani," anasema.

Jambo lingine ambalo mtaalamu huyu anashauri ni kujenga nyumba inayokidhi mahitaji yako.

Kwamba ni muhimu kufahamu ni nyumba ya aina gani unayotaka kujenga kwa kutazama mahitaji yako katika uhalisia wa sasa na wa baadaye na kumshirikisha mtaalamu aliyebobea katika usanifu wa nyumba za kuishi.

"Kujenga kwa kuzidi mahitaji yako, inaweza leta hasara ya kushindwa kumaliza ujenzi. Unaweza ukajiuliza maswali kadhaa, Je, kuishi kwenye hiyo nyumba ni faida zaidi kuliko kupanga?,ni muhimu kuhakikisha kwamba unajenga kwa faida na si hasara.


"Baadhi wamejikuta wamejenga nyumba ambayo inadumu kwa muda mfupi, wapo waliofikiri kutumia vifaa duni vyenye gharama ndogo ndiyo namna ya kupunguza gharama na badala yake walijikuta wakihitajika kuvibadili baada ya muda mfupi na kwa gharama kubwa zaidi.

Wapo pia waliochakachua kwa kujua kwamba ndio njia nzuri ya kupunguza gharama, na kujikuta katika hatari za nyufa, kubomoka na kutokudumu kwa muda unaofaa. Hakikisha unakuwa na mtazamo wa kiuchumi wa kujenga kilicho bora, imara, kinachodumu na kwa gharama nafuu," anasisitiza.

Ally anasema kwamba kabla ya kuanza ujenzi wa nyumba yako, ni vizuri pia ukadodosa na kupata taarifa sahihi zinazohusiana na ujenzi ikiwamo gharama ambazo hutumika kulipa mafundi, vifaa vinavyopaswa kununuliwa ili kukusaidia kufanya uamuzi bila hofu na usionekane hujui chochote mbele ya mafundi wako na wakatumia mwanya huo kukudanganya baadhi ya vitu.

Na anashauri pia kuhakikisha unasimamia ipasavyo ujenzi wa nyumba yako unapoanza hadi unapomalizika ili kuhakikisha kila kitu kinakwenda kama kilivyopangwa badala ya kuwaachia huru mafundi.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
MSHAWAHI KUMTWISHA?
NDIO MAANA UNAAMBIWA KICHWA CHA NYOKA HAKIBEBI MZIGO!
SIO WAKATI WA KUCHIMBANA... UKIMUONA MTU KALA SUTI ALAFU HANA KWA KWENDA "PIGIA MSTARI"
HAPO KWA "KUPIGIA MSTARI" FAFANUA
HA HA HAAA!!! SASA NIME-GUNDUA KUWA DAGAA MBOGA!
MSITUYEYUSHE NA KINGEREZA CHENU KIBOVU!
KIZUNGU GANI KIMEJAA ZE ZE ZE...OFU KOZI NYINGIIIII!!!
DEREVA HAWA WASITUCHANGANYE PAKI GARI BAR TUJIBU MAPIGO.
HAWA WATAKUWA WAMEYACHAPA MAJI, SASA KIZUNGU HEWA KINAWATOKA!
GERE YA NINI?! NA NYIE SI-MKASOME INGLISHI KOZI?
HII NGOMA SIJUI NANI ATAIONA KAMA NAICHEZA KWA MBINDE!
RIBA-MIKOPO
KADRI NINAVYO-ZUNGUSHA RAUNDI NA AKILI NDIVYO INAVYOZUNGUKA!
HUJA-TUMWA "SANDA" KWELI?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
SAMAKI USIMKAANGE NA MAFUTA KIDOGO ATAUNGUA MKIA...

# Raia Kherson wajimwaga mitaani kushangilia

**KYIV,** UKRAINE

WANAJESHI wa Ukraine wamekaribishwa kwa furaha mjini Kherson na wakaazi waliojawa na furaha, baada ya Russia kuthibitisha imejiondoa kikamilifu katika mji huo muhimu wa kusini.

Video ilionyesha wenyeji wakiwa mitaani wakipeperusha bendera ya taifa ya Ukraine na kuimba huku wanajeshi wa nchi yao wakiwasili.

Wengine waliimba nyimbo za kizalendo karibu na moto mkubwa uliowashwa kwenye kambi.

Kherson ilikuwa mji mkuu wa kikanda pekee uliochukuliwa na Russia baada ya uvamizi wa Februari. Kurudi nyuma kumeonekana kama moja ya vikwazo vyake katika vita.

Russia ilisema wafanyakazi 30,000 wametolewa nje ya eneo hilo pamoja na vipande karibu 5,000 vya vifaa vya kijeshi, silaha na mali nyingine.

Ikulu ya White House ilisifu kile ilichokiita ushindi wa ajabu, huku Rais wa Ukraine Zelensky akiitaja kuwa ni siku ya kihistoria.

Lakini waziri wa mambo ya nje wa Ukraine alisema vita vinaendelea.

Akizungumza nchini Cambodia kando ya mkutano wa kilele wa nchi za Asia, Dmytro Kuleba alisema: "Tunashinda vita vya chinichini, lakini vita vinaendelea."

Taarifa ya jioni ya juzi kutoka upande wa Ukraine ilisema kuwa wanajeshi walikuwa wamesonga mbele hadi ukingo wa magharibi wa mto Dnipro.

Picha pia ziliibuka zikionyesha kuwa kivuko kikuu cha mto huo Daraja la Antonivsky, limeporomoka kwa kiasi. Bado haijafahamika jinsi uharibifu huo ulivyofanyika. Wanajeshi wa Russia walioikalia Kherson wanafikiriwa kuchukua nafasi mpya upande wa mashariki wa mto.

Mkazi wa Kherson alielezea hisia zake zinazoelemea, wakati watu walipoibuka wakiimba na kucheza barabarani.

Alexei Sandakov ambaye alifichua jina lake kamili kwa BBC, alisema Kherson ilikuwa huru sasa na kila mtu alikuwa akilia tangu asubuhi.

Aliongeza kuwa kila mtu alitaka kukumbatia askari wa Kiukreni walipowasili.

Mabadiliko ya udhibiti wa jiji hilo yalifuatia shambulio la haraka la Kiukreni katika miezi ya hivi karibuni.

Katika hotuba yake ya jioni ya jana, Rais Zelensky alisema watu wa Kherson walikuwa wakisubiri na hawakukata tamaa.

Aliongeza kuwa wakazi wamekuwa wakifanya kazi ya kuondoa athari zozote kutoka barabarani, zikiwemo nembo za Kirusi.

Wakati huo huo, msemaji wa Rais wa Russia Vladimir Putin, alikanusha hatua hiyo iliwakilisha kushindwa kwa aibu.

**BBC**



Mtoto akicheza kwenye mabaki ya nyumba iliyoathirika na viwango vya juu vya bahari iliyoharibu nyumba kadhaa zilizojengwa kwenye ufuo na kuwalazimu wanakijiji kuhama huko El Bosque, nchini Mexico. **PICHA: REUTERS**

# Mapigano makali yaendelea DRC

**KINSHASA**, DRC

WAKAZI wa jimbo la kivu kaskazini, mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo wamesema kumekuwa na mapigano makali kati ya waasi wa M23 na jeshi la serikali.

Jeshi la serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, wiki hii lilitumia helikopta na ndege za kivita kulilenga kundi hilo.

Waasi hao wanadhaniwa kuhusika na uvamizi dhidi ya shule sita za msingi na kupora akiba ya chakula.

Ghasia hizo zimechangia kuzorota kwa uhusiano baina ya Congo na Rwanda.

Kila upande ukituhumu mwenzake kwa kuunga mkono makundi tofauti ya waasi. Tuhuma ambazo pande zote zinakana.

Jitihada za kidiplomasia zinaendelea katika kurudisha uhusiano baina ya nchi hizo mbili jirani.

Rais wa Angola Joao Lourenco, amerudia nia yake ya upatanishi. Jitihada zake zinaonekana kuwa muhimu kusitisha maelfu ya watu wanaolazimika kuyaacha makazi yao kwa kutoroka vita.

Wanajeshi wawasili DRC

Wanajeshi wa Kenya, wamewasili jana katika mji wa Goma Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kama sehemu ya ujumbe wa amani wa kikanda katika eneo hilo linalokumbwa na mapigano.

Kulingana na shirika la habari la AFP, bunge la Kenya liliidhinisha kupelekwa kwa wanajeshi zaidi ya 900 katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambapo uasi wa kundi la M23 umezua hali ya wasiwasi wa kikanda.

**BBC**

## Guterres asema ulimwengu umeshindwa

**NEWYORK,** MAREKANI

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, amesema ulimwengu umeshindwa katika wajibu wake kwa nchi ya Myanmar.

Alisema matumaini yake kwa Jumuiya ya Mataifa ya Kusini-Mashariki mwa Asia ASEAN kuwa itaweza kuishinikiza nchi hiyo mwanachama wake kuzingatia mpango wake wa amani katika kipindi cha mwaka ujao yamefifia.

Juzi wakati wa mkutano wa kilele wa jumuiya hiyo unaoendelea huko Phnom Penh, viongozi wa jumuiya hiyo walikubaliana kuhusu mpango unaoweka jukumu kubwa kwa Indonesia itakapochukuwa uenyekiti.

Alielezea Myanmar inatakiwa kutekeleza kile kinachojulikana kama makubaliano ya pointi tano kwa ajili ya amani.

Uamuzi huo wa jana pia unajumuisha ombi kwa Umoja wa Mataifa na washirika wengine wa nje la kusaidia juhudi za kundi hilo.

Guterres alisema ana tumaini kwamba balozi maalum wa Umoja wa Mataifa kwa Myanmar Noeleen Heyzer atashirikiana kwa karibu na wenzake wa ASEAN kumaliza ukiukaji wa haki za binadamu nchini humo.

**DW**

## Uturuki yamteua balozi Israel

UTURUKI imemteua balozi wake atakayekwenda nchini Israel baada ya miaka minne ya kuvurugika kwa uhusiano wa kidiplomasia.

Vyombo vya habari nchini Uturuki vimeripoti kuwa Sakir Ozkan Torunlar, mwanadiplomasia mkongwe ambaye aliwahi kuwa ofisa anayeiwakilisha Uturuki nchini humo kati ya 2010 na 2014, aliteuliwa kwenye wadhifa huo kutokana na agizo la rais lilotolewa juzi.

Uturuki ilimuondoa balozi wake nchini Israel mwezi Mei 2018 na kumfukuza balozi wa Israel kuhusiana na hatua ya jeshi la Israel ya kuwauwa Wapalestina kadhaa.

Israel nayo ikajibu kwa kumfukuza balozi wa Uturuki mjini Jerusalem.

Uhusiano kati ya mataifa hayo mawili ulidorora baada ya Rais wa Uturuki Recep Tayyip Erdogan, kukosoa sera ya Israel dhidi ya Wapalestina chini ya serikali za awali za Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu, aliyerejea tena madarakani.

Lakini Erdogan alituma barua ya pongezi kwa Netanyahu baada ya ushindi wake katika uchaguzi uliofanyika mwanzoni mwa mwezi huu.

**DW**

MAKALA

# NJIA ZILIZOONDOA UKABILA ZITUMIKE KUJENGA UADILIFU



Na Magabilo Masambu

KUNA namna mbalimbali za kujenga jamii. Lakini katika makala hii nitazungumza mbili. Moja ni juu ya kujenga jamii kupitia falsafa. Njia hii inahitaji muda na maandalizi ya muda mrefu. Si jambo linaloweza kuchukua muda mfupi kueleweka, lakini ikiwa litaeleweka na kukaa mioyoni mwa watu, kulivunja kwake itakuwa kazi ngumu sana.

MWALIMU Julius Nyerere, mwasisi wa taifa la Tanzania, kwa namna mbalimbali, alijenga falsafa ya kuondoa ukabila Tanzania. Njia mojawapo aliyoitumia ni kutumia lugha ya Kiswahili kutuunganisha. Haikuwa kazi rahisi kwa sababu lazima yako makabila ambayo yangetamani kutumia lugha zao kama lugha za mawasiliano kati yao na makabila mengine. Kwa hiyo halikuwa jambo dogo kubadilisha aina hiyo ya fikra.

Leo Tanzania tunazungumza lugha moja, tunajitazama kama watanzania na si kama Wakurya, Wajita, Wasukuma, Wakwele au kabila lolote lile. Ni kazi iliyochukua muda mrefu, lakini ikaleta mafanikio makubwa na ya kudumu. Leo ni kazi ngumu sana kuvunja falsafa hii ya kutokuwa na ukabila. Mtu yeyote anayeonyesha kuwa ni mkabila hata wa kabila lake pia hawamtaki. Vipi wa kabila lingine si ndiyo kabisa? Kwa hiyo kupanga ni kuchagua, ikiwa tutataka kutumia njia fupi za kurekebisha tabia za watu au njia ndefu ambazo zitadumu milele.

Njia ya pili inayotumiwa kujenga jamii fulani ni sheria mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Katiba ya nchi. Sheria huwa inatumika pale makosa yanapokuwa yamejitokeza. Kwa maana nyingine, sheria haitumiki kuzuia makosa, bali inatumika kuhukumu makosa lakini hukumu hizo zikikusudia kuogofya wengine ili wasitende makosa hayo. Wakati wa ukoloni sheria ngumu na kali zilitumika kuogofya watu na wakati mwingine watu walinyongwa hadharani, ili kuwafanya wanaotarajia kufanya makosa kama yale, kuogopa lakini bado hilo halikufanya watu wasitende makosa.

Ukiitazama jamii yetu kwa sasa, tunaweza kukubaliana kwamba kwa kutumia sheria kali itaweza kupunguza tu kasi ya watu kufuja na kuiba fedha za umma, lakini halitakuwa suluhisho na sababu yake ni kwamba mtazamo wa jamii nzima umebadilika. Wezi na wafujaji wa mali za umma ndio mashujaa mtaani na wale ambao ni waaminifu wanaonekana washamba. Licha ya ushamba, mara nyingine wamekuwa maadui kazini, hivyo kufifisha juhudi za wachache hao ambao wangeliweza kujenga nchi yetu.

Kwa maana nyingine, tunaweza kusema inawezekana wale tunaopiga kelele kuhusu wizi na ufisadi juu ya mali za umma, wengi wetu si wanufaika wa wizi huo, ndiyo maana tunapiga kelele na kwamba ikiwa nasi tutapata nafasi hizo, pengine tutazitumia, huo ndiyo mtazamo wetu kwa sasa. Hili ni jambo hatari sana kwa maendeleo ya taifa. Tukishakuwa na jamii inayoamini kwamba wizi ni kazi nzuri kuliko haki na uadilifu, basi maendeleo ya nchi tutasubiri sana kwa sababu watu wanaingia kwenye mfumo wakiwa waaminifu, lakini baada ya muda wanabadilishwa na kuwa wezi.

Kuna umuhimu mkubwa kama taifa, tuanzishe utafiti juu ya sababu zinazofanya watu wasiwe waadilifu katika utumishi wa umma. Utafiti huo utasaidia kuleta utatuzi wa tatizo kuliko kuwa na hisia kwamba labda ufujaji unafanyika kwa sababu hizi na zile. Lakini wakati tukiangazia utafiti wa kisayansi, wakati huo huo tuone namna bora ya kujenga jamii upya kimtazamo ili tusitumie sheria kama utatuzi wa matatizo tuliyo nayo.

Kuna askari mmoja katika nchi fulani, akiwa kwenye moja ya maduka makubwa (supermarket) akifanya doria, alimwona mama mmoja akiiba mkate na kuuficha ili aondoke nao. Askari alichofanya, alimsogelea na badala ya kumkamata kama mwizi, alimuuliza kwa nini ameiba mkate? Yule mama akamwambia kwamba ameiba mkate kwa sababu nyumbani watoto wake walilala njaa siku kadhaa. Alichokifanya yule askari ilibidi amnunulie mikate mingi zaidi kuliko kumkamata na kumpeleka jela.

Kuna umuhimu mkubwa wa kujua kwa nini watu wanaiba ingali wengi wao wana mishahara mikubwa. Tukijua hilo, utakuwa mwanzo wa kutafuta njia za kutatua tatizo. Sikatai kuhusu sheria kutumika kutoa adhabu kwa wahalifu lakini kama tukiweza kuzuia makosa kufanyika kwa kuwafundisha wanajamii pamoja na viongozi kwamba fursa wanazozipata si za kujitajirisha, bali kujenga nchi na kusaidia wananchi wenzetu, basi huko mbeleni hatutakuwa na matatizo makubwa kama sasa.

Tuwafundishe watoto wetu kutoka ka ngazi ya familia kwamba kikipatikana kidogo ni kwa ajili yetu sote. Tusipokee mahindi mabichi nyumbani wakati hatuna mashamba wala hatujawapatia fedha za kuyanunua. Tusiwafurahie watoto wetu wanaoanza kazi leo, kesho wana maghorofa na magari ya kifahari bali tuwaulize wapi wanatoa fedha hata kama zile fedha zinatusaidia.

Tukishafanya hivyo na ikawa tabia baadaye utakuwa utamaduni na mwisho wa siku, litakuwa kama jambo la ukabila Tanzania na kila atakayekuwa anajaribu kuvunja utaratibu huo, awe adui yetu sote kama ambavyo adui wa sasa kwenye maeneo ya kazi ni yule aliye mwaminifu na mwadilifu juu ya mali za umma.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Franco, Kida walivyowachana mawifi wenye vidomodomo



Na Adam Fungamwango

**"Hivi ni kwa nini dada zetu hamuwapendi wake zetu? Mungu ametengeneza hiki kitu, ni kwamba hakuna mwanamume anayeweza kumuoa dada yake. Mwanamke atatoka mbali na kuolewa na kaka yako."**

ZAMANI hata mimi nilidhani tabia ya baadhi ya wanawake kutowapenda wake za kaka zao ni hapa Bongo tu.

Baada ya ujio wa filamu za kiNigeria nilifuta hayo mawazo kwani nao baadhi ya filamu zao zilionyesha kuwa tatizo hilo liko hata huko. Nikajua labda tatizo hili lipo barani Afrika tu. Baada ya kuingia kwa tamthilia za Kichina, Kifilipino, Kihindi na zingine za mashariki ya mbali, ndipo nilipojua kuwa kumbe ni tatizo la dunia nzima. Nadhani ni la kiasili tu.

Ni kweli kabisa kama tunavyoshuhudia kwenye tamthilia nyingi, baadhi ya ndugu wanaume hasa wa kike, huwa hawawapendi wake wa kaka zao. hapa wsanaitwa mawifi.

Mara nyingi wanawake ambao wameolewa hupata tabu sana kwenye ndoa zao kutokana na dada za waume zao.

Tatizo hasa ni nini? Kama nilivyoeleza mwanzo hili ni tatizo la kiasili. Wadada wanamfahamu kaka yao tangu wako wadogo. Na hata anapokuwa mkubwa na kupata kazi, kinadada ndio wanapata pesa na kununuliwa zawadi mbalimbali. Kaka anaweza kuwapa dada zake pesa ili wapike chakula. Lakini anapoingia mwanamke mwingine hapo mambo yanabadilika. Ataanza kuweka utaratibu wake. Na kwa hali ya kawaida mapenzi ya mwanamume yatakuwa yamehamia kwa mkewe, kiasi kwamba kaka atapunguza baadhi ya vitu na zawadi ambazo alikuwa wakiletea na kuwapa dada zake.

Hapo ndipo mambo yanapoanza. Kinadada wanaona msichana mmoja tu ambaye hata hatujui alipotoka anakuja kubadilisha aina yao ya maisha waliyozoweshwa na kaka yao. Kama walikuwa wanapata hata pesa ya kwenda saluni sasa hawapati tena. Hapo ndipo zengwe linapoanza. Mke atapigwa zengwe hadi nyumba ataiona chungu.

Nadhani wale wanaotazama sana tamthilia hizi wameshakutana nayo sana. Hii ni hali halisi kabisa kwenye jamii zetu. Asili ya mwanamke ni kuwa na mamlaka nyumbani kwake. Hata akiwa na miaka 18 tu, anapoingia kwenye nyumba na kuwakuta wifi zake ambao kwa umri ni wakubwa, na si hao tu hata shemeji zake, ili mradi tu nyumba ile mwenye sauti ya mwisho ni mumewe, basi atatengeneza utaratibu wa yeye ndiye awe anaikotroo kila kitu.

Kama walikuwa wanapika wenyewe, basi hawatoruhusiwa kupika mpaka yeye aamuru na kila kitu kitafanyika chini ya amri yake na si tena kama zamani.

Hili ni jambo la asili kabisa kwa mwanamke na huwa hawafundishwi na wako sahihi kabisa. Kuna mwanamke mmoja aliwapiga marufuku majirani kuangalia televisheni nyumbani kwake mara baada ya kuolewa. Kabla ya hapo mumewe alikuwa akiwaachia ufunguo majirani ili wawe wanakwenda kufungua nyumbani wake na kuangalia televisheni. Tabia ilikoma baada ya jamaa kuoa.

Katika kuonyesha kuwa jambo hili lipo kwa baadhi ya mawifi, mwanamuziki Mkongomani, Lwambo Luanzo Makiadi Franco, mwanzoni mwa miaka ya 1980 alitoa kibao chake kiiywacho '12,600 Letters.' Ni kwamba anadai kupata barua 12,600 kutoka kwa wanawake wanaowalalamika kunyanyaswa na mawifi zao.

Katika wimbo huo ulioimbwa na lugha ya Kilingala na tafsiri yake fupi inasema hivi.

"Hivi ni kwa nini dada zetu hamuwapendi wake zetu? Mungu ametengeneza hiki kitu, ni kwamba hakuna mwanamume anayeweza kumuoa dada yake. Mwanamke atatoka mbali na kuolewa na kaka yako, sasa kwa nini huwa mnawasumbua? Mungu anataka kaka aoe mke akatengeneze familia yake na dada aolewe akakae na mumewe nao watengeneze familia yao." Katika hizo barua ambazo baadhi amezisoma anasema mwanamke mmoja aliyeandika barua kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo alimlalamika kuwa alipoolewa alimkuta mumewe anaishi na kaka na dada zake. Kasheshe ilikuwa wakati wa kupika kwani mawifi walimkaza na kumwambia wao ndio watampikia kaka yao.

Mwingine anaitwa Isuma kutoka Congo Brazaville. Yeye anadai aliolewa lakini kwa sababu hakujaliwa kupata mtoto kwa muda mrefu, mawifi wakamlazimisha kaka yao kuoa mke mwingine shoga yao ili amzalie watoto. Hizi ni baadhi ya barua alizozisoma Franco zingine zikiwa na vituko kwenye kushangaza na kuhuzunisha.

Hayati Hemed Maneti mwishoni mwa miaka ya 1980, alitunga kibao ambacho pamoja na yeye kuimba, lakini kwa asilimoa kubwa kiliimbwa na mwanamama Kida Waziri. kikaitwa 'Wifi Zangu Mnaninyanyasa."

"Vituko na matusi ndani, matusi na maneno nyimbani kwa kweli ni jambo la kushangaza, mtu na wifize kugombana. Tunachogombana sikijui, hivyo yanibidi niyavumilie mimi. Pengine ni mavazi jamani, pengine Jumamosi tunavyotoka.

Lakini jamani yakizidi, itanibidi mimi niondoke sababu ni kwamba sipendelei, na wifi zangu tugombane.

Kuwasema naogopa, kwani nitagombanisha. wifi zangu mna mambo, mambo yenu ya ajabu, jamani nifanye nini? Naelewa mazoea yana tabu, nitajitahidi kusahau.

Kwanza mngejiuliza nini ananipendea, mnadhani miti shamba, na mapenzi hayana dawa. Jamani nifanye nini?"

Haya ni mashairi yaliyomo kwenye wimbo huo. Mke anawauliza mawifi, 'kwanza mgejiuliza, nini ananipendea?' Hapo tu. Mawifi mnalo? Mjibuni basi.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaji, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele. Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi imevunjika-5

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HADI wakati huo Jerry hakuwa ameongea kitu chochote kile. Kwa sababu kwanza hadi anafika hapo hakuwa anajua ameitiwa nini. Na bado mpaka sasa alikuwa anatafakari jambo hilo na hajapata maamuzi kichwani mwake.

Hata hivyo, alichokasirika moyoni mwake ni kuona mambo yanajirudia. Vayajo alimtoroka siku ya harusi. Alipa hatokwenda tena kule. Mzee Mbegu amemwita na baada ya tafakari ya kina akaamua kwenda. Anakutana tena na kitu kama hicho.

Binti anakataa tena mbele yake. Hilo pia lilimkumbushia machungu aliyoyapata siku alipotaka kufunga ndoa.

"Nimeitwa tena kutiwa aibu? Kwa nini wasingekuwa na uhakika na hili ndiyo waniite?" Ni swali ambalo angeuliza kama isingekuwa ni heshima ya sehemu ile ambayo yeye aliichukulia kama ukweni.

"Mimi nadhani hakijaharibika kitu. Nadhani niwaachie tu mjadala uendelee na chochote mkiwa tayari mtaniambia. Kama shemeji ataendelea na msimamo sawa, na kama hatoendelea nao si vibaya ni uamuzi wake na wala msimlazimishe. Nadhani sasa wewe nenda kampumzike." Jerry alimaliza utata huo kwa hekima, hakutaka malumbano au majibizano ambayo yangeleta sintofahamu.

*****************************

"Haiwezekani, haiwezekani, yaani mimi sikubali kutaka kuniulia mwanangu. We mama mchawi, nani asiyekujua kijiji hiki. Kijiji chote cha Msangani watu wanakufahamu kwa tabia yako. Unaruka na ungo usiku. Leo unataka kuniulia mwanangu kisa kamkataa mwanao?"

"Mama Vayajo usinichefue, mwanao kama kagongwa na nyoka mmepeleke hospitali siyo kuleta zako za kuleta. Mwanamke badala ya kukaa nyumbani kumpikia mumeo, we kiguu na njia kueneza uzushi na umbea tu."

"Wee! Nani mbeya?"

"Wewe uliyetoka kwako kuja huku..."

Ilibidi itumike kazi ya ziada kwa baadhi ya watu waliokuwa wamekusanyika hapo kuwadhibiti wanawake hao wawili waliokuwa tayari wameshapandisha hasira na kutaka kupigana.

Walifanikiwa kuwadhibiti kutaka kupigana na si midomo yao. Waliendelea kutupiana maneno ya dharau, jeuri, kila mmoja akiongea kitu ambacho anaamini kitamchoma mwenzake.

Ugomvi huo ulizuka baada ya Zulfa kugongwa na nyoka alipokwenda shambani kuchuma kisamvu kwa ajili ya chakula cha mchana mita chache tu kutoka nyumbani.




**Ugomvi huo ulizuka baada ya Zulfa kugongwa na nyoka alipokwenda shambani kuchuma kisamvu kwa ajili ya chakula cha mchana mita chache tu kutoka nyumbani.**

Kugongwa kwake kukazua mtafaruku kwani mama yake aliwaacha wanaume wamshughukie binti yake kwa huduma ya kwanza na matibabu mengine, yeye akaingia ndani ya kuchukua kanga yake, akafunga kiunoni na kwenda kwa mwanakijiji mwezake, mama Said.

Wiki moja iliyopita mama Zulfa alipata taarifa kuwa binti yake aliambiwa 'utaona' na mama Said baada ya kumkataa kijana wake.

Taarifa hizo alipenyezewa na jirani yake mmoja ambaye aliliona na kulisikia tukio hilo.

"Mama Vayajo, nimekutana na mama Said anamnanga binti yako Zulfa, anamwambia una nini wewe unamkataa kijana wangu Said? Ungemkubali tungekupa shamba, nyumba, hao wazazi wako hawana lolote. Sasa kama umemkataa utaona."

Mama akambana binti yake akamthibitishia. "Ni kweli mama Said alikuwa ananitaka, nikamkataa, nikamwambia mimi hapa nimekuja tu mara moja, sijapazoea sana, nimekulia Morogoro, sitaki kuwa na penzi yoyote wala kuolewa hapa Kibaha, akaenda kumwambia mama yake.

Kuna siku nikaja kuitwa hapa, nikapelekwa kwao, mama na dada zake wakanibembeleza wee, lakini msimamo wangu ukawa pale pale. Ni kweli mama, siku hiyo nilikutana naye natoka kisimani, ndiyo akaniambia maneno hayo."

"Sasa mbona hukuniambia mama yako?"

"Niliogopa, nikaona utakwenda kugombana naye bure."

Baada ya wiki moja, leo yanatokea hayo. Zulfa anagongwa na nyoka. Mama yake akarudisha kumbukumbu zake nyuma. Akaona ajali hiyo ina mkono wa mtu. Akafunga kibwebwe na kumfuata mama Said akifuatana na ndugu zake wengine.

"Yaani asirogwe binti yako aliyetuchezesha ngoma hapa, akakimbia kuolewa, akamkimbia mume mchana kweupe mbuzi anakula majani, arogwe huyo kwa kipi hasa.

Kijana wa watu mbona hajakwenda kwa mganga. Kwanza mimi siyo mchawi na hata kama ningekuwa nao, nisingekuwa na uchawi wa kuchezea kiasi hicho." Mama Said alizidi kuchachamaa, akiwa na uhakika kuwa sheria ni yake kwa sababu amefuatwa nyumbani.

"Namwambia hivi, binti yangu apone yule, akifa maiti yake naileta hapa hapa uwanjani kwako mchana kweupe uile nyama." Mama Zufla alipayuka kwa hasira, lakini wakati huo ndugu zake wengine ambao hawakupenda ugomvi na kitendo kile walikua wamemfuata na walikuwa wameanza kumrudisha nyumbani.

**********************************

Alichukua kipande cha mnofu wa kuku na kukitia mdomoni. Akachukua mkate nao akautafuna. akanyanyua kikombe cha chai akaimywa. Wakati akifurahia utamu, na vyakula hivyo vikitumbukia tumboni, akasikia mlio wa simu yake.

Ilikuwa ni saa mbili usiku Jerry akiangalia taarifa ya habari. Alilazimika kuingiza mkono wake mfukoni ambao ulikuwa na mafuta yaliyogandia kutokana na kushika paja la kuku alilokuwa anakula. Kutokana na shauku ya kujua ni nani hakutaka kupangusa na karatasi laini iliyokuwepo mezani wala kunawa na maji.

Ghafla akakunja sura alipoona namba ya mtu huyo ambaye simu yake inalia. Akaiweka mezani. Hakutaka kupokea kabisa. Akikumbuka kisa cha kuitwa Kibaha na kwenda kuambiwa mambo ambayo aliona yasingewezekana, hakutana tena kusikia habari za huko. Ni sehemu ambayo ilikuwa chungu kwake. Hakutaka hata kuisikia.

Ikakata, lakini baada ya dakika mbili ikapigwa tena. Akili nyingine ikamjia kuwa apokee, lakini akatae atakachoambiwa. Ilikuwa ni namba ya mzee Mbegu. Akabonyeza kitufe cha kupokelea. Haraha akaanza yeye kusalimia

"Shikamoo babu."

"Marahaba mjukuu wangu, habari za siku mbili tatu?"

"Nzuri mzee, wanasemaje huko?"

"Aaah bwana huku habari siyo nzuri." "Eee, unasema?"

"Habari huku siyo nzuri shemeji yako Zulfa ameumwa na nyoka."

"Duh, kweli babu siyo habari nzuri hizo, enhee ilikuwaje na mmempeleka hospitali?"

"Mjukuu wangu, tumetumia dawa za kienyeji hapa, tumemchanja, tumefanikiwa kutoa sumu, sawa kwa hilo limefanikiwa, lakini sasa naona mguu kama umeanza kubadilika rangi unakuwa mweusi."

"Hee, sasa babu mmemuwahisha hospitali?" "Wakwe zako na ndugu wamempeleka kwa mganga wa kienyeji, wanasema amerogwa."

"Mama yangu, watamkosa huyo mtoto au binti anaweza kuukosa mguu wake mkileta mchezo, huyo apelekwe hospitali."

"Nina nguvu hiyo mjukuu wangu? Labda uje wewe unisaidie."

INAENDELEA JUMAPILI





# 50 CENT KUIGIZA KAMA HUSHPUPPI

MWANAMUZIKI mkongwe wa Marekani, 50 Cent ametangaza kuwa anatengeneza msururu wa vipindi vya televisheni kuhusu maisha ya tapeli namba moja duniani Hushpuppi.

Tangazo hilo la 50 Cent limezua mjadala mtandaoni baadhi wakiunga mkono wazo hilo, huku wengine wakisema utawafanya Wanigeria waonekane vibaya.

Hushpuppi ni raia wa Nigeria ambaye amefungwa Marekani kutokana na kuiba pesa nyingi kupitia mtandao na kutajwa kama mtu hatari.

Akituma ujumbe huo kwenye ukurasa wa Instagram, 50 Cent ambaye jina lake halisi ni Curtis Jackson, amesema anajiandaa kufanya filamu hizo.

"Kwa ajili ya walaghai ni lazima nifanye hili, msururu wa Hushpuppy unakuja karibuni!" ameandika

Msanii huyo wa muziki wa rap ana historia ya kuandaa vipindi vya TV, ikiwa ni pamoja na msururu wa maigizo wa Power, ambao kwa mara ya kwanza ulianza kutangazwa mwaka 2014.

Hushpuppi, ambaye jina lake halisi ni Ramon Abbas, kwa sasa anatumikia kifungo cha miaka 11 jela kwa kuwa kinara katika mtandao wa kimataifa wa utapeli.

Hushpuppi alikuwa maarufu kwenye mtandao wa Instagram ambao aliutumia kuonyesha utajiri wake mkubwa kwa wafuasi wake milioni 2.8 ,hadi alipokamatwa mjini Dubai mwaka 2020, na akaunti yake kufungwa.

Kwenye mtandao wa Twitter baadhi ya watu wanaonyesha furaha yao juu ya mpango wa 50 Cent.



# *Lilian Mwasha, MC Pilipili, Flora Mbasha kujikita utalii*

MASTAA mbalimbali wakiongozwa na mtangazaji Lilian Mwasha, Maimartha Jesse na Mc Pilipili, wameamua kumuunga mkono Rais Samia Suluhu kuhamasisha utalii wa ndani kwa kutembelea hifadhi mbalimbali za Taifa.

Mbali na watangazaji hao pia waimbaji Flora Mbasha, Mariam Kilyenyi, Grace Sangija, wameungana kwenye uhamasishaji huo wakishirikiana na Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA).

Akizungumza na BT, mwimbaji Marian Kilyenyi amesema: "Tumeamua kumuunga mkono Rais Samia katika kutangaza utalii wa ndani na sasa tumeanza kutembelea mbuga ya Tarangile mpaka sasa hivi tupo huku lengo likiwa jamii ipende kufanya utalii kwenye mbuga zetu,"

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAG KUMUUZA MAGUIRE

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag anataka kumuuza mlinzi wa England, Harry Maguire msimu ujao wa joto na huenda klabu hiyo ikalazimika kukubali chini ya pauni milioni 80 kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Guardian).***

### DEPAY KUONDOKA BURE

MSHAMBULIAJI wa Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28, ambaye amekuwa akihusishwa na uwezekano wa kuhamia Tottenham Hotspur na klabu ya zamani ya Manchester United, anataka kuondoka Barcelona kwa uhamisho wa bila malipo Januari. ***(Mundo Deportivo via Express)***

### MBAPPE NA PSG

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23 amesema anataka kuandika jina lake katika vitabu vya historia vya klabu ya Paris St-Germain ya nyumbani kwake badala ya kuhamia nje ya nchi ili kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Sports Illustrated)***

### JOAO KUBAKISHWA

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone amesema anataka mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix abaki klabuni hapo, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kuhusishwa na Paris St-Germain. ***(Fichajes)***

### AKARIBISHWA CHELSEA

CHELSEA wamemkaribisha mshambuliaji wa Palmeiras mwenye umri wa miaka 16 Endrick na familia yake kwenye uwanja wao wa mazoezi wakijaribu kuzishinda Paris St-Germain na Real Madrid katika usajili wa Mbrazil huyo. ***(Mail)***

### TIELEMANS ATAKIWA

ARSENAL wanapanga kumnunua kiungo wa kati wa Leicester City na Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25 na kiungo wa kati, Danilo mwenye umri wa miaka 21, anayechezea Brazil na Palmerias, Januari. ***(90 Min)***

### AWANIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inapanga kumnunua mshambuliaji wa Shakhtar Donetsk na Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Arsenal. ***(Football Insider)***

### RITCHIE KURUHUSIWA

KLABU ya Newcastle United itasikiliza ofa kwa winga wa upande wa kushoto wa Scotland, Matt Ritchie Januari, huku kocha Eddie Howe akiruhusu klabu kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 kuondoka. ***(Football Insider)***

### ATAKIWA BOURNEMOUTH

KLABU ya Bournemouth inachunguza uwezekano wa kumnunua aliyekuwa kocha mkuu wa Leeds United, Marcelo Bielsa mwenye umri wa miaka 67, kuchukua nafasi ya kocha wa kudumu baada ya kutimuliwa kwa Scott Parker Agosti. ***(Athletic)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAKIMI: RAMOS BEKI BORA DUNIANI

**PARIS,** Ufaransa

**Ni baada ya kutemwa katika kikosi cha timu ya Hispania kwenda kombe la Dunia...**

ACHRAF Hakimi amemtaja Sergio Ramos kama "beki bora zaidi duniani" baada ya mchezaji huyo kuachwa nje ya kikosi cha Hispania kwa ajili ya Kombe la Dunia la 2022.

**Kocha mkuu wa Hispania, Luis Enrique alitangaza uteuzi wake wa wachezaji 26 Ijumaa kwa ajili ya michuano ya kombe la Dunia inayofanyika nchini Qatar, huku Ramos akikosekana baada ya kuwa sehemu ya orodha ya muda ya wachezaji 55.**

Beki huyo wa kati wa zamani wa Real Madrid ameichezea Hispania mara 180, na alikuwa sehemu ya timu iliyoshinda Kombe la Dunia la 2010, na pia mashindano ya Ulaya 2008 na 2012.

Baada ya msimu wa kwanza wa kusumbuliwa na majeraha katika klabu ya Paris Saint-Germain kufuatia kuhama kwake kutoka Santiago Bernabeu mwaka 2021, Ramos tayari amecheza mechi 19 msimu huu.

Hata hivyo, kufuatia habari kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 hataelekea Qatar, mchezaji mwenzake wa klabu Hakimi, ambaye atawakilisha Morocco kwenye michuano hiyo, aliandika kwenye Twitter: "Sergio Ramos. Beki bora duniani.".

Hapo awali Ramos aliachwa nje ya kikosi cha Hispania kwa ajili ya Euro 2020 baada ya msimu wa mwisho wa majeraha akiwa Madrid, huku mechi yake ya mwisho ya kimataifa ikicheza dhidi ya Kosovo Machi 2021 katika kufuzu kwenda Qatar 2022.

Majina mengine ya hadhi ya juu yaliyoachwa kwenye kikosi hicho ni pamoja na David De Gea wa Manchester United, beki wa Athletic Bilbao, Inigo Martinez na Thiago Alcantara wa Liverpool.

Katika mkutano na waandishi wa habari wakati wa kutaja kikosi chake siku ya Ijumaa, kocha Enrique alieleza: "Nina sheria ya kutozungumza kuhusu kukosekana. Hii hutokea kwa makocha wote.

"Sitawahukumu wale ambao hawamo kwenye orodha. Nawashukuru wote waliocheza, muhimu zaidi ni 26 waliopo."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
FULHAM
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 3.59
X | 3.59
2 | 1.92

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARTETA APANGA KUINGIA SOKONI JANUARI



**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amepongeza kiwango cha timu yake katika kipindi cha kwanza cha msimu huu na kufungua milango kwa wachezaji wapya katika dirisha la Januari.

Washikabunduki hao jana Jumamosi walicheza dhidi ya Wolves, ambao ulikuwa ni mchezo wa mwisho kabla ya Kombe la Dunia.

Kikosi cha Arteta tayari kimezidi matarajio ya mapema msimu huu, na changamoto ya nne bora ndio lengo, lakini ukosefu wa kina ndani ya kikosi unaweza kuwa shida hapo mbeleni.

Arsenal wamehusishwa na uhamisho mkubwa soko litakapofunguliwa tena, huku ripoti zikisema dau la zaidi ya pauni milioni 50 limetolewa kwa ajili ya Mykhalo Mudryk wa Shakhtar Donetsk, huku kukiwa na tetesi za kutaka kumnunua Facundo Torres wa Orlando City na Danilo wa Palmeiras.

Ingawa Arteta amethibitisha shughuli kwenye soko iko kwenye ajenda.

"Baadhi ya wachezaji na uzoefu walionao sio mkubwa zaidi, lakini tumeshindana kwa njia ya kuvutia hadi sasa na namba tulizonazo," alisema Ijumaa.

"Ni kweli tunaweza kuiboresha timu, tutakuwa tukitafuta kufanya hivyo kama klabu, dirisha hili halitabiriki hasa michuano ya Kombe la Dunia ikiwa katikati, tutaangalia na kujitahidi kukifanya kikosi kuwa imara zaidi.



## Walker hayuko fiti kwa Kombe la Dunia

**LONDON,** England

KYLE Walker ataelekea Kombe la Dunia bila mechi yoyote ndani ya wiki sita baada ya kuondolewa kwenye pambano la Manchester City na Brentford jana Jumamosi.

Beki huyo wa kulia wa England hajacheza tangu alipouguza jeraha la paja ambalo lilihitaji upasuaji kwenye mchezo wa dabi dhidi ya Manchester United Oktoba 2 mwaka huu.

Hilo halijamzuia kutajwa katika kikosi cha kocha, Gareth Southgate kwa ajili ya michuano hiyo nchini Qatar itakayoanza kesho Jumatatu.

Kiungo wa kati wa City, Kalvin Phillips pia amejumuishwa licha ya kurejea tu kutoka kwa kukaa nje kwa miezi miwili kufuatia kufanyiwa upasuaji wa bega katika mechi ya katikati ya juma ya Kombe la Carabao dhidi ya Chelsea. Hapo awali alikuwa amecheza dakika 14 pekee za soka msimu huu.

Kocha wa City, Pep Guardiola alisema: "Ulimwona Kalvin kwenye mchezo uliopita, yuko tayari. Kyle - bado."

Guardiola hana wasiwasi kuhusu kuhusika kwa yeyote kati yao baada ya matatizo yao ya hivi majuzi ya utimamu wa mwili.

Y | CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 13/11/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4530 | Atalanta vs Inter | 2.88 | 3.52 | 2.23 |
| 15:00 | 5035 | Paris St Germain vs AJ Auxerre | 1.13 | 7.80 | 15.26 |
| 16:00 | 4899 | Dynamo Kiev vs Kolos Kovalivka | 1.31 | 4.78 | 7.99 |
| 16:00 | 5953 | Shakhtar Donetsk vs Zorya Lugansk | 1.43 | 4.47 | 5.64 |
| 16:00 | 5984 | Horsens vs Odense | 2.69 | 3.38 | 2.46 |
| 16:30 | 5839 | Groningen vs Fortuna Sittard | 2.03 | 3.46 | 3.36 |
| 16:30 | 5966 | Austria Klagenfurt vs RB Salzburg | 5.62 | 4.65 | 1.41 |
| 17:00 | 1418 | Montpellier vs Reims | 2.45 | 3.33 | 2.73 |
| 17:00 | 1983 | Nantes vs AC Ajaccio | 2.00 | 3.18 | 3.83 |
| 17:00 | 2244 | Verona vs Spezia | 2.08 | 3.32 | 3.36 |
| 17:00 | 2688 | Lille vs Angers | 1.31 | 5.20 | 8.40 |
| 17:00 | 2969 | Brest vs Troyes | 2.05 | 3.53 | 3.29 |
| 17:00 | 3341 | Istanbulspor vs Hatayspor | 2.32 | 3.29 | 2.94 |
| 17:00 | 3385 | Monza vs Salernitana | 2.06 | 3.31 | 3.41 |
| 17:00 | 3950 | Brighton vs Aston Villa | 1.81 | 3.56 | 4.05 |
| 17:00 | 5027 | Roma vs Torino | 1.88 | 3.31 | 4.06 |
| 17:30 | 3721 | Mainz vs Eintracht Frankfurt | 2.68 | 3.38 | 2.43 |
| 18:00 | 2805 | CD Algar vs Celta Vigo | 29.76 | 18.85 | 1.01 |
| 18:45 | 3184 | Feyenoord vs SBV Excelsior | 1.12 | 8.15 | 14.91 |
| 19:00 | 1951 | Stromsgodset vs Bodo Glimt | 5.41 | 5.21 | 1.43 |
| 19:00 | 2061 | Valerenga vs Molde | 2.84 | 3.98 | 2.12 |
| 19:00 | 3714 | Lamia vs Panetolikos | 2.16 | 3.20 | 3.40 |
| 19:00 | 4056 | LASK Linz vs Sturm Graz | 2.36 | 3.39 | 2.62 |
| 19:00 | 5422 | Genclerbirligi vs Eyupspor | 4.00 | 3.56 | 1.76 |
| 19:05 | 2027 | Strasbourg vs Lorient | 2.14 | 3.42 | 3.17 |
| 19:30 | 1633 | Fulham vs Manchester Utd | 3.59 | 3.59 | 1.92 |
| 19:30 | 2438 | SC Freiburg vs Union Berlin | 1.99 | 3.22 | 3.76 |
| 19:30 | 5265 | Slask Wroclaw vs Legia Warszawa | 3.21 | 3.25 | 2.08 |
| 19:30 | 5288 | HNK Rijeka vs Dinamo Zagreb | 5.65 | 4.28 | 1.45 |
| 19:30 | 5911 | Cukaricki St vs FK Mladost Gat | 1.29 | 4.86 | 8.35 |
| 20:00 | 2954 | Nordsjalland vs Aalborg | 1.68 | 3.84 | 4.59 |
| 20:00 | 3674 | AC Milan vs Fiorentina | 1.68 | 3.76 | 4.55 |
| 20:00 | 5732 | Besiktas vs Antalyaspor | 1.57 | 3.99 | 5.39 |
| 20:00 | 5750 | Doxa Katokopia vs Apoel Nicosia | 5.60 | 3.80 | 1.59 |
| 20:30 | 1765 | Anderlecht vs Racing Genk | 2.64 | 3.39 | 2.49 |
| 20:30 | 2786 | Olympiakos vs AEK Athens | 2.29 | 3.18 | 3.09 |
| 20:30 | 5468 | CD San Roque vs Getafe | 12.94 | 5.97 | 1.20 |
| 21:00 | 2164 | Casa Pia Atletico vs GD Chaves | 2.04 | 3.28 | 3.58 |
| 21:00 | 3684 | CD Cazalegas vs Real Sociedad | 30.03 | 19.02 | 1.01 |
| 21:00 | 3915 | Portimonense vs Sporting Braga | 4.78 | 3.73 | 1.67 |
| 21:00 | 4874 | Benfica vs Gil Vicente | 1.13 | 7.98 | 15.96 |
| 22:00 | 4067 | Randers vs Midtjylland | 2.89 | 3.49 | 2.26 |
| 22:00 | 4222 | GO Ahead Eagles vs Vitesse Arnhem | 2.39 | 3.38 | 2.73 |
| 22:30 | 2040 | PAOK vs Volos | 1.47 | 4.18 | 6.37 |
| 22:30 | 4104 | Panathinaikos vs Atromitos | 1.37 | 4.38 | 8.37 |
| 22:45 | 1137 | Monaco vs Marseille | 2.30 | 3.48 | 2.83 |
| 22:45 | 4072 | Juventus vs Lazio | 2.00 | 3.27 | 3.65 |
| 23:00 | 2038 | Kortrijk vs KAA Gent | 4.67 | 3.82 | 1.67 |
| 23:00 | 4675 | UD Alzira vs Athletic Bilbao | 14.87 | 6.54 | 1.17 |
| 23:30 | 3987 | Famalicao vs Sporting Lisbon | 4.99 | 3.74 | 1.65 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# MINZIRO SASA ALIA MVUA ILIWANYIMA POINTI TATU

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la timu ya Geita Gold limesema kwamba, mvua iliyonyesha wakati wa mchezo dhidi yao na timu ya KMC iliwavurugia mahesabu yao.

Akizungumza jana baada ya mchezo huo, mkuu wa timu ya Geita Gold, Fred Minziro alisema walitarajia kupata pointi tatu, lakini mvua iliwafanya watoke sare ya 1-1.

> **"Tulitarajia kupata pointi tatu, lakini mvua ambayo ilinyesha imetufanya tupate sare tukiwa kwenye uwanja wetu wa nyumbani," alisema Minziro.**

Kocha huyo alisema baada ya kuona mvua inazidi alibadilisha mfumo waliokuwa wanautumia wachezaji wake na kuwapa mfumo mwingine.

Alisema mchezaji wake Juma Luizio ambaye alikaa nje kipindi kirefu akiendelea kufanya mazoezi ni miongoni mwa wachezaji tegemezi ndani ya kikosi chake.

"Juma Luizio juzi alicheza mchezo wake wa kwanza baada ya kukaa kipindi kirefu ameonesha uwezo mzuri na endapo akiendelea kufanya mazoezi atakuwa miongoni mwa wachezaji tegemezi," alisema.

Alisema baada ya mchezo huo anajipanga kwa akili ya michezo mingine iliyopo mbele yao.



Mchezaji wa timu ya NSSF Veterani, Hamis Msumi, akiwatoka wachezaji wa timu ya vijana wanaolelewa na Kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete, wakati walipokuwa wakicheza mechi ya kirafiki jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Bodi yajiuliza upungufu

INATOKA UK. 24

jani," alisema Kasongo.

Alisema wamekutana na viongozi wa timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu kuhusu kanuni ambao umekuwa mjadala uliochukua muda mrefu.

"Wajumbe wamekubaliana wawe na tabia ya kuzisoma mara kwa mara, kukumbushana wao viongozi na wachezaji ili kupunguza makosa na kupewa adhabu za mara kwa mara," alisema Mtendaji Mkuu huyo wa Bodi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Steven Mguto, alisema katika tathimini yao pia wanaangalia jinsi gani ya kusaidia timu za Championship na Ligi Daraja la kwanza kuepukana na hali ngumu na kushindwa kumudu mahitaji.

Alisema baadhi ya timu zilitaka kujitoa kutokana na kushindwa kujimudu, wameona itakuwa vyema, bodi kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kulitafutia ufumbuzi.

## *Yanga kazi ile*

INATOKA UK. 24

wake wanatembea na matokeo miguuni.

"Mchezo utakuwa mgumu, tumejipanga na tunazitaka pointi tatu, kuhusu mambo ya kiufundi sitowapa nyinyi ila nitawapa vijana wangu.


"Ukicheza na timu hizi kama za Simba au Yanga ambazo wachezaji wake wanatembea na matokeo kwenye miguu yao, lazima ucheze kwa tahadhari sana. Nawapa hongera sana Yanga wamecheza na 'Waarabu' wamepiga mwingi, lakini sasa waje huku wakutane na 'waswahili' wenzao, sisi hatuna majeruhi, wachezaji wote wapo vizuri na tumesafiri na wachezaji wote kutoka Kagera," amesema Mexime.

Timu hiyo ipo kwenye nafasi ya 12 kwa pointi zake 11, hivyo inahitaji kuondoka eneo hilo na kusogea juu kidogo.

# Michezo

Jumapili Novemba 13, 2022

Nipashe


Hakimi: Ramos beki bora duniani UKURASA 21




Wachezaji wa Yanga, Kibwana Shomari (kushoto) na Yannick Bangala wakiwa mazoezini. **PICHA: YANGA**

## Bodi yajiuliza upungufu wa mashabiki

**Na Saada Akida**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), ipo katika mchakato wa kupata mshauri wa kufanya tathmini ya kupungua kwa watu uwanjani na kushuka kwa mapato ya mlangoni katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hivi karibuni wakuu wa idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba na Yanga waliwasisitiza mashabiki wao kwenda uwanjani kwa wingi kushuhudia timu zao zinapocheza huku Azam wakitumia njia ya mashabiki anayevaa jezi ya timu hiyo kuingia bure.

Katika hatua hiyo Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almas Kasongo alisema idadi ya mashabiki uwanjani imepungua na bodi ipo katika kufanya tathimini na kutafuta ufumbuzi wa sababu ya watu kutoingia uwanjani kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Alisema kuhusu mapato ya mlangoni wanaendelea kutafuta ufumbuzi wa kudumu, wakiwa katika kipindi cha mpito na hivyo wanatakiwa kutafakari na kuangalia jinsi ya kupunguza viingilio.

"Tumekubaliana tutafute mshauri atakayetusaidia kujua sababu inayowafanya watu wamepungua kwenda uwanjani kisayansi, tumeweka wazi mapato na idadi ya watu walioingia kila klabu ili ijue ina kazi gani ya kufanya na kuhakikisha zinawashawishi mashabiki kuingia uwan-

INAENDELEA UK. 23

# *Yanga kazi ile ile kwa Kagera Sugar*

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Yajipanga kufikisha mechi 46 bila kupoteza leo, Nabi asema wamejipanga...

WAKIWA bado na furaha waliyoipata baada ya kuichapa Club Africain bao 1-0 ugenini nchini Tunisia na kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho la soka Afrika, CAF, Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara Yanga, leo watashuka kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza kucheza dhidi ya Kagera Sugar ambao ni wenyeji wa mechi hiyo.

**Mechi hiyo itachezwa ikiwa ni siku nne tu tangu ilipocheza mechi hiyo ya mchujo kwenye jiji la Tunis na kuandika historia ya kutinga hatua ya makundi ya kombe hilo baada ya misimu minne.**

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi amesema wanakwenda kucheza mechi ngumu kwani tangu Kagera Sugar ilipobadilisha mwalimu imeonekana kuimarika.

Nabi pia alilalamikia uchovu wa wachezaji wake akisema wametumia muda mrefu wakiwa angani kuliko ardhini.

"Katika kila mechi ya timu kubwa kama Yanga ni kujiandaa kikamilifu na kumheshimu mpinzani unayekwenda kucheza naye. Tumejiandaa na mechi hii ingawa ni kwa shida sana kwani tumetumia muda mrefu kwenye ndege kuliko kwenye ardhi, hilo ni tatizo kwa afya ya wachezaji, mchoko, lakini hatujaja hapa kulalamika, tumejiandaa na mechi tuna deni kwa mashabiki wetu.

"Tutoe wito kwa viongozi wenye mamlaka, sisi tumekwenda kuiwakilisha Tanzania, tusiadhibiwe kwa hili, tunaamini hili halitojitokeza tena," alisema Nabi.

Yanga ambayo si tu kwamba ndiyo timu pekee ambayo haijapoteza mechi yoyote msimu huu hadi sasa, lakini haijapoteza michezo 45 hivyo kama itapata ushindi au kutoka sare itafikisha mechi 46 na kuzidi kutengeneza rekodi ya aina yake.

Itakuwa ni mechi ya tisa kwa Yanga ambayo ina pointi 20 hadi sasa na kabla ya mechi ya Simba dhidi ya Ihefu iliyochezwa jana usiku, ilikuwa ikiongoza ligi.

Hata hivyo, itakuwa ni mechi ya 11 kwa Kagera Sugar ambayo kwa sasa ipo chini ya Mecky Mexime baada ya hivi karibuni kumtimua kocha wake Mkenya, Francis Baraza kutokana na mwenendo mbaya wa timu.

Akizungumzia mechi hiyo, Mexime alisema mechi itakuwa ngumu kwa sababu wanacheza na timu ambayo wachezaji

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >